

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

KILGORIS CONSTITUENCY, HELD

AT EMURA DIKIRR SEC SCH

ON

17TH JULY, 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS – RIFT VALLEY PROVINCE KILGORIS CONSTITUENCY AT
EMURA DIKIRR SEC SCH ON WEDNESDAY 17TH JULY, 2002**

Present

Com. Dr. Charles Maranga - in the chair

Com. Abida Ali Aroni

Secretariat staff in-attendance

Ismail Aden - Program Officer

Omwanza Ombati - Assistant Program officer

Flora Wafula - Verbatim Recorder

Ole Seiwa - District Co-ordinator

The meeting was called to order at 10.20 a.m. It started with a word of prayer from the Pastor.

Com. Maranga: Sasa ningeita Pastor mmoja kutoka pande hii yetu ya Emura Dikirr atufungulie mkutano kwa moambi. Pastor ako wapi? Bwana Seiwa, tuko na pastor gani hapa? Pastor chukua hii microphone. Jameni tusimame kwa maambi.

Pastor: Natuombe. Toeni kofia wazee.

Baba kwa siku ya leo tunakuja mbele yako, tukiwa na asante, maana ametuleta pamoja. Bwana Tumeamini utakuwa na sisi wakati tunaongea hapa, Bwana tunajua kwamba unatujua, asante hata kwa wale wako njiani Bwana, tunawaomba upate kuwaongoza, pia tunakushukuru kwa wale umeweza kuleta Bwana, kwa safari jema, tunakushukuru kwa hio Bwana. Pia na sisi utuongoze ili mwishowe tuweze kukushukuru. Nimeomba nikiamini kwa jina la Yesu Kristo aliye mkombozi wetu.

Com. Maranga: Nafikiri benches ziko hapa na watu wanaweza kuketi kwa hivi viti, na pengine ningemwiita Bwana Co-ordinator, kuna DCs hapa ambaye ungetaka ku-introduce? Hawajafika? OK, kwa hivyo sio watu wengi sana. Basi kabla hatujaanaza, pengine nitawajulisha tu, na baadaye nitawaomba tusimame kwa dakika moja kuna mwenzetu ambaye munajua ni first Vice Chairperson wa Commission Dr Ooki Ombaka, ambaye ameaga dunia, kwa hivyo, ningepomba baadaye tusimame kwa dakika moja. Pengine tusimame sasa dakika moja, ili baadaye nitawajulisha ni akina nani wako hapa. Tutoe heshima kwa huyo naibu wa mwenye kiti. (moment of silence) Basi asanteni, na munaweza mukaketi.

Basi ningetaka kuwajulisha ni akina nani tuko nao hapa leo, na ninataka kutangaza mkutano wa Tume ya kurekebisha Katiba, na leo tuko upande wa Emura Dikirr.

Kwanza kabisa, hebu niwajulisha ni akina nani wako hapa. Kwanza kabisa tuko na naibu wa Mwenye Kiti wa Tume Ya Kurekebisha Katiba, Bi Abida-Ali Aroni. Hebu namuuliza awasalimie kidogo.

Bi Aroni: Hamjambo? Tunawakaribisha kwa mkutano wa leo na tunamatarajio mutatokea kwa wingi na kutupatia maoni yatakayo tufaa. Asanteni.

Basi huu ni naibu wa Mwenye kiti wa Tume Ya kurekebisha Katiba, na nataka vile vile kuwajulisha ni akina nani tuko nao kutoka kwa Secretariat ama upande wa Headquarters. Tuko na Bwana Ismail Aden, ambaye ni Program Officer, huyu ndiye atahusika na maneno yoyote ambaye yanahusika na maneno ya Secretariat. Kama una taabu yoyote, huyu ndiye unaweza ukaona mara moja. Wa pili ambaye tunataka tumjulisha ni Bwana Omwanza ambaye ni naibu wa Program Officer. Tunaye vile vile Bi Flora Wafula, huyu ambaye ndiye ananaza sauti zenu, ili aweze akachukua maoni kabisa na huyo ndiye mwingine kutoka kwa Secretariat. Vile vile, nafikiri ningempa Co-ordinator wenu Bwana Ole Seiwa, ndiye huyu, kwa sababu alikuwa hajajitambulisha. Ni Co-ordinator wa upande huu wenu wa Constituency ya Kilgoris. Basi kwa ufupi kabisa, hawa ndio Tumetoka nao kutoka (problem with sound – microphones) CKRC.

Basi, wacha niwaelezee kidogo, vile sisi tulifika hapo hapa awali, lakini tukapata ya kuwa kulikuwa na hitilafu kidogo. Sisi kama watume tulikuwa tumetangaza ya kuwa hio mkutano ilikuwa imeahirishwa, na tukakubaliana tutarudi hapa Jumatano. Leo

ndiyo tuko hapa, hata ingawa mnajua tuko na maombolezi kidogo kulingana na vile mmejua naibu Mwenye Kiti alituaga, kwa hivyo sisi kama Wanatume, tunatakiwa tuwe tumerudi Nairobi hivi karibuni tuone tutafanya namna gani. Lakini hebu niwape masharti yale tutafuata wakati sisi tunatoa maoni mbele ya Tume.

Kwanza kabisa, mtu anajitambulisha kwa jina lake. Unafika kwa Tume, unajitambulisha kwa jina, unasema mimi ni fulani kabla ya kuanza kuongea. Munaona kuna viti viwili hapa, Tumeweka hapo, mtu anaweza akaongea kwa lugha yeyote. Unaweza ukaongea kwa lugha ya Kimombo, lugha ya Kiswahili, ama lugha ya mama. Kwa upande huu, mtu anaweza akaongea kwa lugha ya Kipsigis. Lakini kama unajua Kiswahili, badala ya kungojea mtu atafsiri, ni vizuri unaweza ukaongea kwa ile lugha sisi kama WanaTume tunaweza tukaelewa.

Mambo yenu yote ambayo munaongea, yananaswa na chombo moja ya tape recorder, ama kile chombo ya kunasia sauti. Kwa hivyo hata ukiona Commisioners hatuandiki kila kitu, tunacho chombo kingine kile kinaweza kikachukuwa sauti yako. Hata ukikohoa, kidogo, kinachukua. Vile vile kuna Program Officer hapa. Vile vile wanaandika. Sisi vile vile kama Wanatume, tunaandika.

Kuna njia tatu za kutoa maoni. Njia ya kuanza kabisa, mtu anaweza kufika mbele ya Tume, na anaongea. Akiongea kutoka kwa kichwa chake, yaani hana karatasi ya kusoma ama chochote. Sehemu ya pili ya kutoa maoni, ni unaweza ukatoa nakala ama memorandum mbele ya Tume, mbila hata kuzungumza. Unaweza ukatupatia memorandum na uondoke. Hiyo ni sawa sawa, hio maoni umefika kwa Tume. Na kuna mtu ambaye ako na memorandum, lakini vile vile anataka kughusia ile maneno ya muhimu; hio vile vile tunakubali. Hizo ndizo njia tatu za kutoa maoni. Kuna vile vile wananchi watafika hapa mbele, na wanataka kusikiza. Wanakaa wanasikiza. Hio pia ni sawa sawa. Mtu anaweza akaketi hapa, asikie vile wengine wanaongea. Na kama nakuita kwa jina, na unafikiri maoni yako yametolewa na mwingine, basi una haki ya kusema, nilikuwa nataka kutoa maoni, lakini nafikiri fulani au watu wengine wameongea maoni yangu. Hiyo vile vile unaweza ukafanya. Kwa hivyo na sisi, vile tumepita Kenya mzima, tumeona hivi. Mtu ambaye hana nakala ama hana memorandum ya kutoa mbele ya Tume, tunampa dakika tatu, yaani yule mtu anaongea, mzee anakuja anaketi hapo, anatoa yale maoni, mapendekezo tunampa dakika ngapi? Tatu.

Na yule ambaye ako na memorandum na anataka kutupa ile maneno ya muhimu, tunampa dakika mbili. Munafanya summary, main highlights. Maana tunampa namna hilo ni kwa sababu ile memorandum ukitupa, sisi kama Tume, tutaenda, tutapiga chapa, hio ripoti utaona. Kama wewe unaitwa Bwana Koech, Bwana Rotich, utaona hio report yako yote imekuwa katika ile report ya constituency ya Kilgoris. Kwa hivyo mutaisoma wakati hio report itakuja hapa. Na ni haki yenu kuwa report itafika hapa. Hii ndio njia nyingine tumezungumzia, vile tutafanya. Kwa hivyo itakuwa dakika mbili kwa wale watu ambao wako na memorandum, wanatupa highlights, dakika tatu, kwa wale watu ambao hawana memorandum yoyote. Na vile vile sisi kama Wanatume, tunaweza tukakuuliza maswali ama utuelezee zaidi pendekezo lolote umetoa. Na tena kitu kingine munatakiwa kujua sisi hatutaji majina ya watu. Kama unataka kuongea kuhusu Ofisi ya Rais, usitaje jina la Rais; unataja Ofisi ya Rais.

Kama ni Ofisi ya Chief, hata ikiwa Chief amesumbua wewe namna gani, usitaje yeye Chief fulani, jina fulani. Unasema Ofisi ya Chief ningetaka iwe namna hii. Tumesikilizana kwa hio maneno? Kama ni polisi ambao wanasumbua nyinyi, usiseme polisi fulani kwa jina fulani. Unasema Ofisi ya Polisi ama Idara ya Polisi. Unasikiza haya maneno? Kwa hivyo una uhuru ya kutoa maoni. Na usiwe na wasiwasi hata kama Chief ako, polisi ako, Kila mkenya na haki ya kutoa maoni vile unavyotaka. Na tunataka tutumie ile lugha ambayo hutusi watu, ama ambayo haichanganyishi watu. Wewe kama una maoni kunyume ya mwingine amezungumza, una haki ya kufika mbele ya Tume, na wewe vile vile utoe maoni yako.

Kama mtu anatoa maono ambayo hupendi, hakuna aja ya kupigia yeye makelele ama nini. Hapana. Unakaa kimya, unangojea wakati wako, na wewe useme vile unavyotaka. Tumeelewana? Basi na vile tunavyotaka, tutafuata hii. Kuna listi hapa ambayo sisi Tumepeana hapa. Sijui meza ya ku-register watu iko wapi Bwana Co-ordinator.

Nafikiri ungeweka kuna meza hapo, ama mahali inaonekana wazi kabisa, kando kidogo watoke kando wale watu wanataka kujiandikisha munajiandikisha, sisi tutafuata hii. Na mimi nikiita jina, na wewe huko, basi bahati yako baya, mimi nasonga mbele. Kwa hivyo, mimi nitaita majina hapo ili ndiyo watu waje mbele watoe maoni. Tumesikizana kwa hiyo maneno? Tumesikizana?

Basi, nafikiri kwa hayo machache, mimi nataka tuanze, na tuna muda mfupi wa kutoa maoni leo kwa sababu tunashughuli nyingi, lakini tuliahidi watu wa Emura Dikirr lazima tutafika hapa. Kwa hivyo tuko hapa na tunataka mutoe mapendekezo. Kama unatoa mapendekezo kuhusu kilimo, ama elimu, twambie vile ulisumbuka kidogo, lakini peana pendekezo. Kama ni pande ya maziwa, kama ni mashamba, kama ninini, tupe pendekezo. Usitwambie o sisi watu wa upande wa Emura Dikirr hatuna mabara bara hatuna nini, sasa unataka tufanye nini? Tupe mapendekezo. Ningetaka iwe namna hii. Kama ni uongozi ambayo nyinyi hampendi, munasema sisi tungetaka maneno yetu yafanywe namna hii. Tumesikizana hio maneno? Peana mapendekezo ambayo yatasaidia Tume. Si kutoa tu malalamiko. Tumesikizana? Kwa hivyo watu wakifika mbele hapa, kama ni elimu unaona iko na gharama ya juu, mumeshindwa kulipa fees, basi twambie kama munataka elimu ya bure, ama unataka fees irudishwe chini, ama ni nini munataka. Maneno ya afya, namna hivyo hivyo. Tumesikilizana? Kwa hivyo mupeane mapendekezo. Basi bila kupoteza wakati, nataka kumwita mtu wa kwanza kabisa, Bwana Philip Mutai.

Com. Maranga: Philip Mutai. Ako? Hayuko. Wa pili ni P K Rotich. Rotich ako? Hayuko. Samuel Rabor? Huyu ni ofisa hapo. Benjamin Chepkwony? Hajafika. William Chepkwony? Hajafika. Richard Tonui? Hajafika. David Kimolel? Hawa ni wale walikuja zamani waka register wakati tulifika hapa. Sasa ndio nilikuwa nawaita. Samuel Rabor? Wewe ulikuwa uongee. Unataka kuongea? Basi ketu huko uanze. Wewe unaitwa Samuel Rabor? OK, ingia hapo uongee basi. Uanze kwa majina yako, na uanze na kutuambia ni nini unataka. Unaweza ukaamua usimame ama uketi. Sasa hiyo maoni ni yako. Chaguo ni lako.

Samuel Kibor: Jina langu ni Samuel Kibor.

Com. Maranga: Hebu ongeza sauti hapo madam. Just add all of them. You will know which one is good.

Samuel Kibor: Jina langu nimeandika huko. Sasa mimi ninazungumza habari ya masomo ile tulizungumza hapa. Masomo imetushida kabisa wananchi. Sasa nataka watoto wa secondary wasome. Wasome bila malipo. kutoka secondary, form one. Hio ni maoni yangu.

Com. Maranga: Anayefuata ni Milliam Milgor. Yuko? Kuja.

William Milgor: Kwa majina, mimi naitwa Willima Milgor na ningetaka kutoa maoni yangu kupitia memorandum. Ningetaka kugusa mambo muhimu kwa dakika moja au mbili. Ya kwanza, ningetaka Katiba ya Kenya ijulikane na kila mtu. Wananchi wote wa Kenya wawe chini ya sheria ya Kenya. (clapping)

La pili la muhimu ni sheria ya mashamba. Sheria ya mashamba iwe moja katika Kenya. Kusiwe na sehemu zingine zinaruhusu watu kuchukua shamba kama group. Hizo shamba zichukuliwe na individuals kama iko sheria wakati huu.

La tatu ni kwamba ningetaka masomo yawe ya bure kutoka nursery mpaka secondary level. (clapping)

Ya mwisho, councillors, ama Chairmen wa municipalities wawe wanachaguliwa na wananchi. (clapping) Asanteni.

Com. Maranga: Asante Bwana Milgor. Mimi ningependa hiyo memorandum uandike jina lako, halafu uende upeane. Tunataka hio memorandum. Sasa anayefuata ni Byomido Johnstone.

Byomido Johnstone: Kwa majina ni kama vile umesikia. Byomido Johnstone na nitapitia kwa ufupi memorandum ile nimeandika. Jambo la kwanza ni kuhusu raia. Tulikubaliana ya kwamba wale wananchi wote wamezaliwa katika hii inchi ya Kenya, wawe raia wa Kenya bila kupingwa. (clapping)

Jambo la pili, kuna watoto wamezaliwa kule Nairobi na hawajui wazazi. Street children, pia wawe raia.

La tatu tukasema ikiwa kuna mtu kutoka nchi za nje ambaye anataka kuwa raia, ni lazima apitie njia inayofaa. Sio kupitia vichoro choro.

Kuhusu vyama vya siasa, tukapendekeza ya kwamba, ili tusiwe na vyama vya ukabila, tuwe na vyama kama tano na hivyo vyam viwe vinaweza wawe wanaweza kupata asilimia 15 kwa wale raia wamejiandisha kawa wapiga kura.

Jambo la nne, ni kuhusu serikali. Tukasema ya kwamba tunataka serikali ambayo Waziri Mkuu atasimamia serikali na Rais awe tu ceremonial President asiwe na nguvu nyingi kama sasa. Kufika kwa President, tukasema yakwamba lazima awe amefuzu katika chuo kikuu na awe na record nzuri za tabia.

Tukapendekeza ya kwamba Rais awe anajipinga kwa Bunge. Wabunge wawe na mamlaka kuliko Rais ili awe akishauriwa, ama akichezea kazi, anaweza itwa na wabunge halafu tunachagua Rais mwingine, tusinyanyazwe.

Tukapendekeza pia kwamba ikiwa mtu anataka kupigania kiti cha Rais, awe na umri wa miaka arubaini hadi sitini na anaweza kuchaguliwa mara mbili, miaka mitano mitano na asirudi mara ya tatu. Akimaliza hiyo, aende apumzika, mtu mwingine apate nafasi ya kuingia kwa uongozi.

Kwa upande wa County Council, tukapendekeza yakwamba, Mayor ama Chairman wa County Council, awe na degree na achaguliwe na raia (clapping) Hapo, ndio hawezi kununua watu wachache halafu anumia resources ama anumia rasilimali ya raia kwa njia ile anataka yeye mwenyewe kuhakikisha ya kwamba wale watu waliye mchagua ndio wanakula peke yao kule.

Jambo lingine ni hii basic rights. Kuna hii mambo, watu wanaua watu wengine, tukasema ya kwamba itekelezwe kulingana na vile huyo mtu aliuawa. Kwa sababu hata mbeleni, sisi tukiwa Wakipsigis tulikuwa na Constitution yetu. Mtu akiua mwingine, kuna ile hatua ilikuwa inachukuliwa.

Kuna watu wanaitwa vulnerable communities. Hawa watu walikuwa wanatekelezwa tu na wazungu kwa ajili ya kunyanyasa hawa watu. Lakini kwa sasa, baada ya miaka arobaine sidhani ya kwamba kuna mtu ambaye inawezekana anatakiwa alindwe kushinda mtu mwingine. Raia wote wawe sawa katika nchi ya Kenya, kwa sababu tulipigania uhuru tukiwa moja. Na baada ya hiyo, kuna watu walikuwa waweke sahihi halafu wanaambiwa mtalindwa. Serikali walinde raia sawa sawa. Sio raia wengine wapewe bunduki, halafu wanaenda kupiga wengine kama swara. Hio kazi ya bunduki iende kwa askari, askari walinde raia, na walindwe vile vile. Hizo silaha ziko na raia zitolewe zipelekwe kwa askari. Halafu askari wafanye kazi yao (clapping)

Kuhusu Bunge tukasema wabunge hawastahili kujipatia mshahara peke yao. Kama ni mshahara inaangaliwa, mishahara iangaliwa, mishahara iangaliwe ya wabunge pamoja na ya wafanyi kazi ya serikali na ya walimu, wakati mmoja (clapping)

Kwa Councillors tukasema hawa macouncillors, siku hizi, watu wengi wamesoma katika nchi hii ya Kenya, na hatuoni kwa nini tunachagua watu ambao hata hawajui kuandika majina yao. Elimu yao iwe kidato cha nne ama zaidi. Ili tupate watu ambao wanaelewa shinda za raia.

Umiliki wa ardhi: Tulipendekeza ya kwamba, hata kama mimi arap Biomindo nimetoka hapa, nikipata shamba Mombasa,

wacha mimi niende huko, niishi huko Mombasa. Kwa sababu sikutuma maombi kwa Mwenyezi Mungu nizaliwe huku Emura Ndirir. Kwa hivyo raia wote, waishi sehemu popote wakipata shamba katika nchi ya Kenya, kwa sababu ni moja. Asante sana. (clapping)

Com. Maranga: Asante, na nakuomba kabisa uweze ukatupatia memorandum, tunaweka kwa hii kitabu yetu rasmi. Anayefuata ni John Ng'eno. John Ng'eno its your turn, halafu atafuatiwa na Benard Ngeno. Benard Ng'eno ako? You will be next. Na ningetaka kutangaza hivi, kama kuna wanafunzi wangetaka kuongea mbele ya Tume, basi wajiandikishe, na wapeane hayo majina kwa District Co-ordinator, ili aweze akanipatia, ili niweze nikawasaidia kwa haraka murudi shuleni. Asante.

John Ngeno: Kwa majina, mimi ninaitwa John Ng'eno. Hapa niko na memorandum lakini jambo niko na maoni nataka kutoa kuhusu administration office.

Kuhusu administration office, naomba kwamba Assistant Chiefs waondolewe mbali, na Area Committee ishike hio laini, hata Area Committee wapewe hio mshahara. Ya pili tena, kwa hio office tena, ninaomba hio ofisi ya Chief wapatiwe normal transfer kama wengine, kama walimu (clapping). Wapate transfer waende na hata wazazi wapate maendeleo kwa sababu kuna wengine wananyanya sub location ama kijiji kingine. Kwa hii ofisi tena ninaomba Tume wafanye hii ofisi, ofisi ya DO iishe, Chief aende kwa DC (clapping). Namalizia hapo.

Kuhusu County Councils, nataja ya ya kwamba, Mayor wa County Council achaguliwe na wananchi, na awe mtu ambaye ako na degree. Ofisi ya DC iende barabara mpaka kwa DC hio iende laini.

Ninaguzi kuhusu upande wa mashamba. Upande wa mashamba, kila mwananchi, mahali alizaliwa, akae hapo, ama mahali anapopata shamba, nikifikiria saa hii niende Kisii, nipate shamba Kisii, naishi Kisii. Kwa sababu mimi ni mwanakenya (clapping). Hakuna haja ya kusema huyu alizaliwa hapa na huyu alizaliwa hapa. Jambo ingine ya muhimu nataka kuguzi ni kuhusu upande wa jimbo. Mimi ninasema kwamba hatutaki majimbo. Tunataka tukae kama ndugu, kila mahali. Kenya ni Kenya. Hakuna kutoa jimbo. Rift Valley tumetolewa, tukae Rift Valley. Mimi sina mengi ya kusema.

Com. Maranga: Asante Bwana Ng'eno, nakuomba utupatie hio memorandum yako, na uweke sahihi kuonyesha kuwa umefika mbele ya Tume. Benard Ng'eno? Atafuatiwa na Ezekiel Sang. Ezekiel ako? Uwe tayari mzee. Anza kwa majina.

Bernard Ngeno: Kwa jina, najulika kama Benard Ng'eno. Na yafuatayo ni mapendekezo kutoka kwa kikundi kimoja ambacho kinajulikana kama Paralegal. Kitu cha kwanza katika kuibadilisha Katiba ya Kenya, tuliona kwamba Katiba ya sasa, haina preamble kama Katiba za nchi zingine. Na katika upande huu wa preamble, tulionealea kwamba preamble ya Constitution ya Uganda, ni nzuri. Na contents za preamble hiyo, ziwe reflected katika Constitution yetu ya Kenya. Except where the contents in link, the preamble of Uganda should be linked to Kenya. Cha pili, tuliangalia tena Katiba ya sasa

Chapter 2 ambayo inaongea mambo ya Rais, na tulionelea kwamba, the Presidential system of Government should be replaced. Tuwe na Prime Minister ambaye atashikilia position ambaye President alikuwa anashikilia. Na pia tuwe na President ambaye atakuwa ni ceremonial President. La muhimu tena katika Chapter hiyo ya pili ni Section 14 of the current Constitution ambayo ilikuwa inamlinda President asipelekwe kotini hata akifanya kosa lolote, civil offences. Hiyo iwe repealed completely.

La tatu tuliangalia tena Chapter 3, Parliament na sitataja mambo mengi kuhusu Parliament hapa. Nimeandika.

Ifuatayo ni Chapter 4 ambayo inaongea mambo ya mahakama, Judiciary. Jambo muhimu katika hii (problem – failure of the public address system) Chapter ya nne katika Constitution ya sasa, tulionelea tubadilishe Chief Justice. Chief Justice awe anachaguliwa bungeni na kwa sababu huyu ndiye atakuwa akishughulikia mambo ya justice.

Katika Chapter hio hio, part 3, Judicial Service Commission iwe established na maofisi ya ofisi hiyo tena wawe wakichaguliwa huko bungeni. Chapter 5, Protection of Fundamental Rights, and freedom of the individual. Hapa hakuna mabadiliko makubwa. Kile kitu kinatakiwa ni kwamba, Katiba itakayo kuja, ihakikishe kwamba imekuwa implemented, This side, we have the best provision. Tuko na provision nzuri sana katika Chapter 5 ya kuangalia mambo ya haki za binadamu. Lakini shida ni kwamba, watu wenyewe hawaelewi haki zao.

Com. Maranga: Last point?

Ni kwamba ingawa sijaandika hapa nilikuwa nataka tena niongeze, kwa kusema mambo ya sheria iwe examinable, ifunzwe katika mashule. Na hata ikiwezekana, iwe examinable mpaka form 4. Na wale watu ambao wanataka ku-extend, ama ku-pursue, with Law Education, waende sasa wafanye hiyo Law university lakini hiyo iwe ikifanywa na wanafunzi wa Kenya ili tusiwe na shida kila mara tunaona uvunjaji wa sheria. Asante sana.

Com. Maranga: OK, thank you very much, nakuomba uweke sahihi kwa kitabu chetu, na utupatie hiyo memorandum yako. Ezekiel Sang? Na mimi ningetaka kutangaza hivi, wale watu ambao wanaingia saa hii, kuna mahali tunafanya registration, kama hata unataka kuwa officer hapa, kuna mahali tunajiandikisha, kwa hivyo, mtu asije akakaa hapo halafu ajiulize ni saa ngapi Wanatume wataniita niongee. Haya, Bwana Ezekiel Sang, anza kwa majina yako.

Ezekiel Sang: *En kainet ko Ezekiel Sang*

Translator – Kwa majina naitwa Ezekiel Sang,

Ezekiel Sang: *Ola mengunen ko Dikir.*

Translator – Anaishi hapa Emura Dikirr.

Ezekiel Sang: *Kit ne atese mising*

Translator – Kitu anaongeza sana,

Ezekiel Sang: *Ko ng'alek ab kechamien ke igun akenge.*

Translator – ni maneno ya amani. Tupendane na tuwe kitu kimoja.

Ezekiel Sang: *Amun mi bik alak en nguenyduni ingot ko kokonyo ng'atutieni koik ngatutiet ne kararan kemache ke ng'alal komie.*

Translator – kwa sababu kuna watu wengine dunia hii, na kwa sababu hii Katiba inakuja kwa njia nzuri, tunataka kuongea vizuri.

Ezekiel Sang: *Amun en ngatutiet ne komi komi bik alak che kegere ko koseretiotin.*

Translator – Kwa sababu hii ni Katiba ilikuwako, watu wengine walikuwa na taabu sana.

Ezekiel Sang: *Ko en inguni*

Translator – Kwa sasa.

Ezekiel Sang: *Amache amwa ale en ng'alek ab ng'alek che kikuren che ba kabesiet ko makimuche kepye Rift Valley makipyee.*

Translator – Amesema kwamba hatutaki Rift Valley igawanywe iwe mara mbili au zaidi.

Ezekiel Sang: *Yache koik akenge.*

Translator – Inatakikana iwe kitu kimoja.

Ezekiel Sang: *Ak chito ne mengisie en ole mengisie,*

Translator – Na mtu mahali anaishi,

Ezekiel Sang: *Ko menye yoton.*

Translator – aendelee kuishi mahali hapo.

Ezekiel Sang: *Kone kimasich en yoton kobur kounoton.*

Translator – Na yule ambaye hakuwa amepata mahali hapo, akae vile alivyo.

Ezekiel Sang: *Amun en ng'atutiet ne kakile ne lel*

Translator – Kwa sababu ya Katiba ambayo anasemekana ni mpya.

Ezekiel Sang: *Oko ko kechamwech kong'alal raia. ni mpya.*

Translator – Na tumekubalishwa kama wananchi tuongee.

Ezekiel Sang: *Ko kit ne mi kora ko,*

Translator – Ilioko tena

Ezekiel Sang: *en ng'atutik chu*

Translator – Ni kwa hii sheria,

Ezekiel Sang: *Ko ng'atutik che lelach.*

Translator – Ni sheria mpya.

Ezekiel Sang: *Ko ngot ko ng'atutik che lelach ako okwek obik che kokikonok oyai kouolemakta bik komatochilil.*

Translator – Na ikiwa ni sheria mpya, na nyinyi ndio mumepewa mufanye kazi hiyo, musifanye kando (clapping).

Ezekiel Sang: *Amun eчек ko kagibwane konyokemwa*

Translator – Kwa sababu sisi Tumekuja ili tuseme.

Ezekiel Sang: *Kakemwa ile ingomwa chi mami chit one kimuche kelenji matimwa kion.*

Translator – Ulikuwa umesema kila mtu aongee, hakuna mtu atakatazwa aongee.

Ezekiel Sang: *Ko kounoton kegase takiigu akenge bik ab Kenya tugul.*

Translator – Kwa hivyo tunataka tuwe kitu kimoja, watu wote wa Kenya.

Ezekiel Sang: *Mi bik alak che lelen takiisto koba yu kole, takista alak koba kole lakini makiyani.*

Translator – Kuna watu wengine wanasema kwamba tunataka watu wengine watolewe hivi, lakini hatutaki.

Ezekiel Sang: *Ak komi ng'aliot age, Majimbo.*

Translator – Kuna neno inaitwa majimbo.

Ezekiel Sang: *Kobaisyen Bik alak kole tamanan ko kimekitun.*

Translator – Kuna watu wengine wanatumia majimbo ili wawe na nguvu.

Ezekiel Sang: *Makiyani Majimbo*

Translator – Hatutaki majimbo.

Ezekiel Sang: *Ngot ko mi kit age ne kewalen Majimbo komakiyani.*

Translator – Kama kuna kitu kingine ya kuweka badala ya majimbo, sisi hatutaki majimbo.

Ezekiel Sang: *Kit ne kang'etyini ko natan ine zaidi kamatindoi ng'alek che chang'.*

Translator – Nilikuwa nashituka sana kwa sababu ya mambo ya majimbo.

Ezekiel Sang: *Mayani Majimbo okot muguledanyun komamache.*

Translator – Mimi sitaki majimbo, hata roho yangu haipendi majimbo.

Ezekiel Sang: *Kongoi missing*

Translator – Asante sana.

Com. Maranga: Asante Mzee wangu. Maoni yako Tumeyasikia. Weka sahihi. You must be around so that you can help us. But lete hio microphone hapa. Josiah Rob. Wapi Bwana Rob. Hayuko? OK karibu. Halafu atafuatiwa na Gladys Kosgey. Gladys? Mama Gladys ako wapi? Gladys ako wapi? Hayuko? John Tanui? Basi uwe tayari. Na wacha nimwambie. Hakuna makosa yoyote kufanya registration kwa hii form. Tunataka vile vile sisi kama Wanatume tujue ni watu wangapi walifika kwenye hiki kikao chetu hapa Emura Dikirr. Kwa hivyo, hata kama wewe hutaki kuongea, unaandikwa observer. Tumeelewana? Hivyo ni kuonyesha ulikuja ukakaa kwa mkutano. Kwa hivyo hakuna makosa. Kwa hivyo watu wafanye registration, hata wanafunzi ambao nimeona wamefika hapa kwa wingi. Hebu explain.

Kagimwa kele chito ake tugul ko lazima isirgei si kor ke nai kele ka bik at ache kabwa yu. Ngot ko me ng'alale isisire kainet ak imwa ile mang'alale. Na wanafunzi sijapata list yenu. Wakati wale ambao wanataka kuongea watakuwa tayari, munielezee. Haya Bwana Rob endelea.

Josiah Rob: Kwa jina naitwa Josiah Rob, na ningependa kutoa sheria kuhusu wanawake. Ningependa kutoa maoni yangu kuwa ninaunga mkono wanawake kwa ugawanaji wa mamlaka katika idara ya serikali au makampuni. Na mambo ya kinyumbani, kati ya mke na bwana, ninaonelea kuwa mwacha mila ni mtumwa. Ningependa kila jamii au kila kabila wafuate sheria zao za zamani. Haitakuwa vyema kuwa usawa kati ya bwana na bibi katika maswala ya kinyumbani. Kwani wanaume wako na kazi nyingi ya kufanya katika mambo ya familia?

Wakulima wanatafuta pesa kwa njia ngumu sana, na pia wanawake wako na kazi zao za nyumbani, za kulima. Hiyo ifuatwe kama jamii mbali mbali wanafanya. Kazi ya watoto wa shule, hasa wasichana: ningependa wapate masomo kama vijana kila mahali, iwe Kipsigis ama Masai ama kabila zingine. Hiyo ninatilia manani sana. Asante.

Com. Maranga: Ngoja kidogo Bwana Rob. Kuna swali.

Com. Aroni: Bwana Rob, ninataka unifafanulie kitu umesema. Umesema kwa sababu yako kutaka kukosa usawa nyumbani, sisemi ni kitu mzuri lakini, hapo mini sielewi. Unasema tusiwe na usawa kwa nyumba kwa sababu wanaume wanafanya kazi ngumu. Ni kazi gani hiyo wanaume wanafanya ambayo ni ngumu kuliko ile wanawake wanafanya kwa sababu kisababu yako mimi nataka nielewe kwa akili yangu.

Josiah Rob: Unajua Bwana Officer,

Com. Aroni: Bibi Officer tafadhali,

Josiah Rob: Bibi Officer, kwa kweli, unajua wanaume wako na kazi nyingi sana.

Com. Aroni: Gani hiyo? Hebu tupatie mifano ya kazi ambayo wanaume wanafanya ngumu sana, na ile sio ngumu sana inafanywa na wanawake.

Josiah Rob: Unajua mwanaume anaweza chimba mawe kiasi kama ile, ili wapate pesa.

Com. Aroni: Akichimba mwanamke ako wapi?

Josiah Rob: Mwanamke anangoja pesa tu iletwe na mwanaume.

Com. Aroni: Hapo katika jamii ya Kipsigis, nani analima? Nani anachota maji? Nani analea? Si ni mama! Siku moja ukipewa hiyo kazi, hebu angalia kama ni ngumu kushinda ya kuchimba mawe. Asante sana. (laughter)

Com. Maranga: Bwana Rob, kuja hapa uweke sahihi na utupatie hiyo memorandum. Gladys Kosgey. John Tanui? Councillor Stanley Langat. Ako?

Basi uwe karibu.

John Tanui: *Kainenyu ko John Tanui.*

Translator: Kwa majina naitwa John Tanui,

John Tanui: *Matinye ng'alek che chang', ng'alek tuten che ang'alali. Amun en ng'alek ab ng'atutichi kagekonech kele kengalalen ii.*

Translator: kwa sababu ya sheria nimeambiwa niongee juu yake,

John Tanui: *Matinye ngalek che chang'*

Translator: Sina mengi.

John Tanui: *Ng'aliondenyun namwae kityo amwae ale,*

Translator: Anasema ya kwamba

John Tanui: *En ng'atutik amun kimwae ng'atutik chukaba Kenya mzima*

Translator: kwa sababu sheria, ni sheria ya Kenya nzima,

John Tanui: *Ke mache keyai ng'atutichu kokimengik ab Kenya.*

Translator: Tunataka tutengeneze sheria tukiwa wananchi ama wakaaji wa Kenya.

John Tanui: *En ng'aliot akenge natindoi.*

Translator: Kwa neno yangu moja ambayo niko nayo,

John Tanui: *Mamache ng'aliot ne kilelen kebe Majimbo.*

Translator: Yeye hataki neno ati unasemekana ati tuingilie mambo ya majimbo.

John Tanui: *Ingemwa ng'aliot ab Majimbo, Kekere kele kagirat kei.*

Translator: Tukisema juu ya majimbo, tunaona ya kwamba tunafungana.

John Tanui: *Mamuche awa ak aker ole kacham en Kenya ak keyetenan.*

Translator: Sio vizuri ati niende nipate mahali pazuri Kenya halafu ninakatazwa.

John Tanui: *Ako a chitab Kenya.*

Translator: Na mimi ni mtu wa Kenya.

John Tanui: *Alen tenachon.*

Translator: Ni hiyo tu.

Com. Maranga: Basi asante Bwana John Tanui, Councillor Stanley Langat.

Councillor Stanley Langat: Asante sana Commisioners and jina yangu ni Councillor Langat.

Com. Maranga: Shika Mic vizuri. Wewe ni kiongozi.

Councillor Stanley Langat: Yangu tu ni oral. Ningetaka kuanzia Local Government. Nataka Chairman wa County Council awe akichaguliwa na watu.

Com. Maranga: Hio mic iko vizuri. Ni wewe hujaiweka vizuri. Unaona wazee wanaongea na wanashika sawa sawa. Ongea sasa.

Councillor S. Langat: Local Government: Chairman wa County Council achaguliwe na wananchi directly. Na awe na kiwango ya elimu ya at least form 4. Pia huyo Chairman, akichaguliwa na wananchi awe na powers kuliko clerk kwa sababu sasa, Chairman huwa chini ya clerk.

Ya pili ni land. Upande ya land, hii maneno ya communal land iwe abolished na iwekwe kuwa individual. Mtu aruhusiwe aishi popote Kenya. Pia maneno ya ardhi, iwe na usawa. Wamawake na wavulana wapewe ardhi sawa katika uridhi.

Pia ningetaka kuzungumzia system of Government, mimi maoni yangu ningependelea tuwe na a strong Executive President, awe na Prime Minister, na ministers, wawe wakiwa mapendekezo tu anapewa President, lakini Bunge iwe inaamua ni nani atakuwa President. Ministers wawe wakisimamia ministries bila kuingiliwa na mtu yeyote. Na wakati anataka kuvutwa, waulize wabunge katika Bunge.

Ya nne ni maneno ya political parties. Maoni yangu ni kwamba political parties ziwe tatu tu. At least 3, na serikali ilipie gharama za matumishi zao. Kwa sababu tumeona hapa Kenya, mtu binafsi anatafuta political party yake, wakati anataka kuhama, anavunja kama ni yake.

Ya tano ni maneno ya Provincial Administration. Maoni yangu ni kwamba, iwe scrapped na nafasi yao ichukuliwe na elected Mayor.

Ya sita ni maneno ya religion. Katika Katiba ningetaka religion iwe ikiangaliwa na serikali kwa sababu wakati huu, watu fulani wanaweza kutumia religion kama njia ya kutafuta pesa, imeingia nyingine hata ya mashetani.

Ya mwisho yangu ni maneno ya education. Tuwe na free education kutoka nursery mpaka form 4, na turudie ile system ya 7-3-4. Asante sana.

Com. Maranga: Asante Bwana Councillor, ningekuomba uweke sahihi na utupe hio memorandum. Hiyo mic unaweza kuweka hapo chini, asante. Samuel Langat? Karibu. Atafuatiwa na John K Tanui. Samuel Langat, kuja haraka haraka. Yule translator wetu ako wapi? Chukua hii mic. Just sit there permanently. Usitoke, uwe unatusaidia hapo. Ongea, anza na

majina.

Samuel Langat: *En kainet kekurenon Samwel arap Langat*

Translator: Kwa majina naitwa Samuel Langat.

Samuel Langat: *Ko en ng'alek ab Katiba ko komieit ke ibyech kora inei asikobit keng'alal bik ab Resob.*

Translator: Kwa maneno ya Katiba, nimefurahia vile imeletwa kwa wananchi.

Samuel Langat: *Ko amun kokeibwech ng'alechu kobwa resob kisachi bik tugul.*

Translator: Na kwa sababu tumeletewa sisi zote, tutaongea juu yake.

Samuel Langat: *Kit ne tai na ng'alalen akane ko ng'alek ab President.*

Translator: Ya kwanza, nitaongea juu ya Rais.

Samuel Langat: *Ko en ng'alek ab President, akere ale machekeger akine President kotinye kasisyek che chang' kikoyum kasisyek che ite somok.*

Translator: Napendekeza kwamba kazi ya Rais ipunguzwe kwa sababu ako na karibu kazi 3 muhimu.

Samuel Langat: *Yani ba newo ne ba majeshi.*

Translator: Yeye ni mkuu wa majeshi,

Samuel Langat: *Oko president ii.*

Translator: yeye ni Rais,

Samuel Langat: *Oko Prime minister*

Translator: Na yeye ni Prime Minister.

Samuel Langat: *Akere ale chang' kasisiek che yae chichon.*

Translator: Anaoma anakuwa na kazi nyingi sana.

Samuel Langat: *Kaigai kegon ne kibare Prime minister.*

Translator: Ni vizuri tuwe na Prime Minister.

Samuel Langat: *Amun katar chichon rabinik che ba bik che chang'*

Translator: Kwa sababu mtu mmoja anamaliza pesa ya watu wengi na pia anakuwa na maneno mengi.

Samuel Langat: *Kanakte awe namba oeng'*

Translator: Naenda nambari ya pili.

Samuel Langat: *Akere kora ale ng'alek ab Majimbo atinye akane kitten.*

Translator: Nataka kuguzia juu ya majimbo.

Samuel Langat: *Akere ale ng'amun ki mengik ab Kenya,*

Translator: Kwa sababu sisi zote ni wananchi wa Kenya,

Samuel Langat: *Oko imbarani kokiba Mungu.*

Translator: Na hii shamba ni ya Mungu,

Samuel Langat: *Ng'o ne kiyae.*

Translator: Hakuna mtu ama binadamu alitengeneza dunia.

Samuel Langat: *Ng'ot ko ng'alal chi kole ne nyon imbarani*

Translator: Kama kuna mtu anasema ati hii shamba ni yetu,

Samuel Langat: *Akase ale kagen.*

Translator: Anaona kwamba anadanganya.

Samuel Langat: *Kiba Mungu.*

Translator: Hii shamba ni ya Mwenyezi Mungu.

Samuel Langat: *Oko kikonu Mungu.*

Translator: Na ni Mwenyezi Mungu ambaye alitupatia.

Samuel Langat: *Ke menye en ole kimi.*

Translator: Kwa hivyo, kila mtu aishi mahali anaishi.

Samuel Langat: *Ng'ot kinam Majimbo,*

Translator: Tukianza majimbo,

Samuel Langat: *Ko keparkei kityo.*

Translator: Ni kuuana tu.

Samuel Langat: *Ingelenjon iba Transmara, oko kimeba Maasaek abaken ne mi Kericho oko mara ko kekoiyot ko maiyani komanda, kepare kei kityo. Memi kiy age.*

Translator: Nikiambiwa ati labda wewe ni mtu wa Trans Mara, na wewe sio wa Trans Mara, ati utoke Transmara uende utoe mwingine Kericho ama pahali pengine, hiyo itakuwa ni vita tupu.

Samuel Langat: *mayani akane ketumda korotik,.....*

Translator: Mimi sitakubali damu imwagwe kwa wananchi.

Samuel Langat: *Lakini chame bik alak any.*

Translator: Lakini kuna watu wanapenda.

Samuel Langat: *Lakini makimuche.*

Translator: Sisi hatutaweza.

Samuel Langat: *Ongemeny chitugul imbarani ba Mungu kotom korarwech.*

Translator: Sisi tuishi wote hii shamba kwa sababu ni ya Mwenyezi Mungu.

Samuel Langat: *Katukyi yon nombo Majimbo.*

Translator: Namalizia hapo juu ya majimbo.

Samuel Langat: *Ko kotom atestai konekit ang'ale kora ng'alek cherubekei ak ngalechu kaba Majimbo che tesetai en bichotet amun kou Transmara. Inang'alal kou korani ne angen.*

Translator: Anataka kuongea juu ya Transmara kwa sababu anajua Transmara zaidi.

Samuel Langat: *Ak angen ale mi oratinwek che kerkei kou Molo.*

Translator: Na mimi ninajua kuna Transmara kama vile Molo.

Samuel Langat: *Amun Molo akine komi kogoyek ak komi Kipsigisiek.*

Translator: Kwa sababu Molo pia kuna Wakalenjin, Wakipsigis na Wakikuyu.

Samuel Langat: *Ko en emet ne mi kabila che chang' ii.*

Translator: Na kwa sehemu kuna watu aina mbali mbali.

Samuel Langat: *Komaribin chitab olatet kou chito neu babangung' ne kisichin.*

Translator: Mtu kama huyo sio kama baba yako ambaye alikuzaa.

Samuel Langat: *Nyalu kochilin en tuguk alak ak kole mang'en okot ole kiibunu.*

Translator: Anaweza kukufinya kwa mambo mengine anakwambia sijui ulitoka wapi.

Samuel Langat: *Ak kole mesom okot ng'echer en korani.*

Translator: Na kusema huwezi hata kuomba kiti sehemu hii.

Samuel Langat: *Abare kiitu*

Translator: Ati wewe ilingia.

Samuel Langat: *oko kokoyanun imengisie mekotwain.*

Translator: Na amekubalia wewe kuishi, hawezi guza wewe.

Samuel Langat: *Akere ale*

Translator: Hii naona kwamba,

Samuel Langat: *Nyalu kindewech kandoindet akenge kerkei ng'ot aba kigoek, ng'ot komi kikoek che mitten Molo, inang'alalen kou oldage ko nyalu kotinye chamchinet kikoek choniton akichek konyo ko ger atebet ab bikyik che miyotet amun maaechin amun chang' Kipsigisiek che mitten Molo ko tuten kikoek ko lazima kechile.*

Translator: Ni vizuri mtu aweze kupewa, kiti chochote akiwa sehemu yoyote, asifinywe mahali hapo.

Samuel Langat: *Ko kakiyaji chito akenge, ng'ot ko kikoek kotinye ne nywan, kikoek kotinye ne nywan kotai komanda lumek.*

Translator: Kila mtu aweze kupata uongozi wawe ni Wakikuyu, Wakipsigis, na watu wengine.

Samuel Langat: *Asikorutechi bikyik ak koteben taabu ne tindoikomakiteben lesienit. Ingebare kemwachin taabu ne nyon kelemen kakonin ng'o rusa.*

Translator: Ili watu wake wawe wakimwendea mbila kuulizwa ulipata ruhusa kutoka wapi.

Samuel Langat: *Akere ale uwon makarara ng'aliondonon kabisa oko tesetai.*

Translator: Hiyo neno si nzuri kabisa na inaendelea.

Com. Maranga: Bwana Langat malizia. Ya mwisho?

Samuel Langat : *Bas alen ko negit atarat any ii, ko maatinye ng'alek che chang' amachekityo ang'alal ne letunen ale kongoi amun kakeibwech ng'alechu keng'lal ra, katata ng'alale lakini katak karor nafasi.*

Translator: Nashukuru sana, naona nafasi imeisha.

Samuel Langat: *Atinye kityo barua ne kayab kokwet oleng'alado.*

Translator: Niko na barua ya kijiji vile waliongea.

Com. Dr. C. Maranya: Asante sana Bwana Langat, atie sahihi, na atupatie hio barua. Anaye fuata ni John K Tanui. Atafuatiwa na Joel Langat. Joel Langat ako? Wapi John? Basi uwe tayari.

John Tanui: Kwa majina naitwa John Tanui, ninatoa maoni yangu. Ya kwanza ni kuhusu mambo ya majimbo. Mimi ninasema hatutaki majimbo. Kwa sababu hiyo majimbo yaliletwa na watu ambao pengine wako na nia yao baya.

Pia nataka kuguzia mambo ya shamba. Shamba ni ya Mungu, hatutaki watu wengine wanasema hati hii shamba ni yetu. Bora tu hajafukuza mtu mahali anaishi. Bora mtu asiwe analalamika.

Pia kuhusu mambo ya election, tunataka Electoral Commission ifuate tunasema hivi.. Siku ambayo uchaguzi utaendelea, tunataka transparent ballot boxes. Pia, tunataka tujue the number of ballot papers ambayo zinatengenezwa wapi. Pia tunataka results zikimalizika, ziwe zinatangazwa hapo, halafu polling stations zingine wapate, kama kwa mfano Emura Dikirr, fulani ameongoza, na hii na hii mpaka hio iishe, halafu izambazwe kwote katika Kenya. Pia ninataka kusema all people should be respected regardless of race, colour or political status. Ninasema hivyo kwa sababu kuna watu wengine wanasema ati kwa vile mimi ninatoka tribe fulani, kwa vile mimi ni mzungu au nini ni lazima niheshimiwe. All human beings should be respected. Whether black or white.

Kuguzia mambo ya preamble, hiyo preamble ndiyo inatakikana kuwekwa katika hii Katiba yetu halafu hata iwe recognised. We should be proud that we are the ones who made this Constitution.

Kuguzia mambo ya jinsia tunataka kusema mambo ya jinsia iangaliwe sawa, halafu tusiwe tunanyanyasa watu wengine. Watu wote ni sawa. Kama mambo ya kazi, wasichana na wavulana wawe wakipewa nafasi sawa.

Com. Maranga: Ya Mwisho?

John K Tanui: Pia nataka kutoa ya mwisho kuhusu viongozi. Kama mtu anataka kuchaguliwa awe MP au awe nini, all his assets, kama ni pesa, ngombe, yote, they should be accounted for and be taken so that when others go there, they do not steal; if anything, they should be recovered kwa sababu watu wengine wanaingia katika siasa wakati ule hana pesa nyingi. Kwa muda mfupi tu, anakuwa millionaire earning the biggest salary. So, kwa Katiba mpya, wanatakikana waelezee the source of their wealth.

Com. Maranga: Asante Bwana Tanui, weka sahihi.

Joel Langat: *Ale in ko kisir memorandam*

Com. Maranga: Wewe mimi naona unaweza kuongea Kiswahili, hata kizungu ukiweza. Wewe ongea Kiswahili. (laughter in the background)

Joel Langat: Tulikuwa tunataka watu wengine wasikie.

Com. Maranga: Hapana. Hii maoni unatoa kwa Wanatume. Tunaelewana. Na wale wazee vile wanakaa kuna wengine wanaelewa, Kiswahili kila mtu anasikia. Kwa sababu wanaendanga Transmara, Kilgoris, wanaongea Kiswahili.

Joel Langat: Tulipokaa tuliandika memorandum kidogo,

Com. Maranga: Anza kwa majina.

Joel Langat: Jina langu ni Joel Langat.

Com. Maranga: Asante.

Joel Langat: Na tulipoandika tukasema kwamba.

Com. Maranga: Tafadhalini mkae kimia kidogo. Hata kama munaketi, mketi pole pole. Haya endelea Bwana Langat.

Joel Langat: Kwa upande ya chief, ma-chief wamesumbuwa wananchi sana kwa sababu wanawekwa na wanasiasa. (clapping) Na tungependa Chief yeyote ambaye anatakiwa katika location, awe anachaguliwa na wananchi. (clapping) Ndio wananchi waamue ni nani atakuwa chief wa hiyo location.

Kwa upande wa security, mambo ya usalama, ni ya kwamba wananchi wengine wasipewe mabunduki na wengine hawana mabunduki (clapping) Kwa hivyo raia wote wawe chini ya serikali moja. Polisi wawe ndio wanasimamia, wanachunga hawa wote, badala ya raia wengine wawe na bunduki na wengine hawana.

Jambo lingine la wasichana, tulizungumza kwamba wasichana ambao watapata shamba katika familia yao ni wale tu ambayo hawajaolewa. Lakini wale wameolewa, wawe watapata mashamba pahali wameolewa. Kwa hivyo, wasipewe shamba kwa

nyumba yao pahali wamezaliwa.

Jambo lingine ni la councillors. Minimum educational requirements iwe ni form 4. Mtu awe amemaliza kidato cha mne. Lakini sio kwamba mtu awekwe kwa County Council ambaye hajui hata kuandika jina lake. Ni jambo la ajabu kwa sababu ameshindwa na kujiongoza, na anataka kuongoza wananchi.

Jambo lingine ni ya kwamba katika sehemu hii tunaishi, tuseme watu makabila mawiili na tungependa ya kwamba hawa Wakipsigis wamekua wengi zaidi, na Wamasai ni wachache na wako na districts kama tatu, Samburu, Kajiado na Transmara, au na Narok, tungependa wasanywe pamoja waamue. Waone mahali wataishi kama ni Samburu au Kajiado, waende huko waishi (clapping). Halafu ndio hawa wengine ambao wamekuwa wengi, wapate mahali pakuishi.

Halafu tena jambo lingine la mashamba, ambayo ilisemekana kwamba mtu lazima aishi mahali ambapo anapenda kwa sababu watu wengine wako na nia nyingine wakisema lazima kuwe na masharti fulani, ndio mtu akae mahali anataka. Lakini sisi tungetaka kusema yakwamba watu wawe na uhuru wa kuishi pahali wanapenda kulingana na vile uwezo wao ulivyo.

Halafu jambo la majimbo, sisi hatutaki majimbo (clapping). Kwa maoni yangu, majimbo yaondolewe kabisa kwa sababu ni nia ya watu wengine. Watu wengine wako na nia baya kuhusu majimbo. Kwa hivyo, kwa maoni yangu, mimi nasema hio iondolewe. Ni hayo tu nilikuwa naye.

Com. Maranga: Asante Bwana Langat. Ninakuomba utupatie memorandum yako. Na uweke sahihi. Sasa ningetaka kuita wanafunzi hapa kidogo, ndio vile vile nao wachangie huu mjadara wa Katiba. Emi Chepkorir. Ako wapi? Atafuatiwa na Betty Chepogeno, nafikiri wangukuja hapa karibu. Halafu Geoffrey Rotich na Bernard Chemiyot. Hawa wanafunzi wafike hapa wote. Wapi Emi kwanza? Kama wako waje wakae hapa karibu, ndio wazungumze moja baada ya mwingine. Na utuambie ni darasa la ngapi ama form gapi, basi Emi Korir. Wewe ninani? Wilson? Wilson mimi sijaita wewe. Subiri kidogo. Kaa nitakuita tu. Haya, Emi? Ongea kwa mic vizuri. Hiyo mic inaongea. Ilete karibu. Haya. Huwezi ukaongea Kiswahili au kizungu?

Translator (name not given): Alikuwa anataka kuongea lugha ya Ki-kipsigis.

Com. Maranga: Sasa wewe, mwanafunzi wa shule darasa la nane. Si uongee Kiswahili? Sasa ukiongea form one utaongea namna gani ukichukukiwa Alliance? Wewe ongea Kiswahili. Huyu ni mwanakenya. Si ulisema waishi Pokot, sema Kiswahili. Ongea na Kiswahili. Ama kizungu. Haya ongea vile unataka. Anza kwa majina.

Emily Chepkorir: *Ane kekurennon Chepkorir Emmy.*

Translator Naitwa Emily Chepkorir.

Emily Chepkorir: *Ayabu sukulit ab lelechonik.*

Natoka shule ya msingi ya Lelechonik,

Emily Chepkorir: *Kilasit sisit.*

darasa la nane.

Emily Chepkorir: *Ne tai amache awekyi kongoi Jehova.*

Anashukuru kwanza Mwenyezi Mungu

Emily Chepkorir: *Ne ba oeng' amache alenjok sigik konyalu osomeshan tibik ko kerkeit ak murenik.*

Translator: Wasichana wasomeshwe sawa na wanaume.

Emily Chepkorir: *Ng'amun tibik ak murenik ak tibik ko kerke tugul lagokuk tug ul.*

Kwa sababu wasichana na wavulana ni watoto wa mtu mmoja na wote ni sawa.

Emily Chepkorir: *Nda Yon kikesich tibik icheken ko to isomeshani ng'o.*

Kama ulikuwa umepata wasichana peke yao, ungesomesha nani?

Com. Maranga: Mwambie aongee kwa mic. Haya endelea.

Emily Chepkorir: *Ne ba oeng' amache alenjok sigik kora komanyalu I lazimisan chepto kowa tumda ile sikobit kobitun tuga.*

Translator: anasema yakwamba wasichana wasilazimiswa kutairi, ili upate ngombe.

Emily Chepkorir: *Neba somok kora ko yon Kasich lakwet ne miten sukul lakwet ko nyalu inamji sikindet lakwet ak kotetai en sukul.*

Msichana kwa bahati mbaya akiwa shuleni mzazi akae na mtoto, Mzazi akae na mtoto na yeye aendeleo na kusoma.

Emily Chepkorir: *Ingap sikai kosich lakwanoton ko sigindet ne ma koi tuguk che yamekei ak lakwet.*

Kwa sababu ni mzazi anaharibu mtoto. Hana vitu via kutosha ndio aweze kukaa mbila taabu.

Emily Chepkorir: *Kachoniton che katindoi.*

Alikuwa tu na hayo. (clapping)

Com. Maranga: Asante na aweke sahihi. OK Betty Chemngeno. Anza kwa majina yako.

Betty Chemngeno: Kwa majina naitwa Betty Chemngeno kutoka shule ya Lelechonik, darasa la nane. Mimi naomba niongee kwa lugha yetu.

Com. Dr. Charles Maranga: Wewe una Kiswahili safi sana. Wewe endelea. Ogea kwa lugha ya Kiswahili. Ni mzuri.

Endelea.

Kitu cha kwanza ninataka kuanzia, ni kuwa nimeshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu ametuwezesha ili tufike wakati huu.

Ya kwanza ni kuwa, kama msichana hakuolewa, ni lazima apewe shamba pamoja na the rest of the family. (clapping)

Kwa kuwa yeye ni mtoto wako. Wewe ndio ulimzaa.

Cha pili, kila mzazi ni lazima asomeshe watoto wake wote. Si ati kusema wasichana wasisomeshe, na wavulana waendeleo.

Na tena sisi kama Transmara tungependa kutoa maoni ya kwamba we are not satisfied with the demarcation of the constituencies vile iko. Ningependekeza kwamba at least, there should be 3 constituencies in a district. Sio moja katika district.

Com. Maranga: Last point.

Richard Tonui : Last point, ningependa tu kupendekeza ya kwamba we adopt the 7-4-2-3 education system ya zamani na iwe free katika primary, cost sharing katika secondary and iwe free also in university.

Pre-school teachers also wale waalimu wa nursery pia wawe wamechukuliwa na serikali na TSC na wasihitaji chochote kutoka kwa wazazi.

Com. Maranga: Thank you very much. Hand over your memorandum and you sign. Kibii Rono, Chebot, is that the collect pronouncialtion, okey, kuna David Bett,

Kibii Rono Chebot: Napendekeza kwamba preamble iandikwe kuleta ile picha inaonekana wasiwasi kulingana na sheria imo ndani. Tena, wale viongozi waheshimu vile imeandikwa kulingana na sheria.

The head of security – ninapendekeza ya kwamba mkuu wa jeshi kutoka kwa askari – General - sio tena akuwe Commander-in-Chief.

Kitu kingine President tena achaguliwe watu Chancellor – sio kuwa Chancellor wa University kuchaguliwe wale wamehitimu kwa kazi hiyo.

Pengine in Parliament, napendekeza serikali iwe President ni ceremonial na head of state (Prime Minister kuwa head of government na judge mkuu – Attorney General achaguliwe na parliament. Halafu Ministry of Justice and Home Affairs iondolewe na hio ofisi iende kwa ofisi ya Attorney General sababu ya Attorney General anafanya kazi ya justice.

Com. Maranga: Ya mwisho.

Kibii Rono Chebot: Napendekeza mambo ya elimu yandikwe kuwa 7-4-2-3 na tena kuanzia primary mpaka secondary kuwa free. Asante.

Com. Maranga: Thank you very much na Rono kuja hapa uweke sahihi Bwana David Bett – halafu ningependa hao wanafunzi wafike mbele – Mary Cherotich, Chepkemoi Florence, Dorcas Kemboi and Faith Chepkurui, mje hapa mbele mkae

hapa karibu na machine zetu hapa za kunasia sauti. Basi kuwa haraka haraka Bwana David Bett. Niko na zaidi ya watu 300, nataka niende haraka.

David Bett: Mimi naitwa David Bett. The 1st proposal I have made nikuwa ya kwamba Katiba yetu iwe na Preamble yenye inaonyesha national vision yaani maono ya kitaifa.

Nyingine we should retain the Present form of government. Hatutaki mambo ya majimbo (clapping).

The people should recall their MP if he does not perform according to their expectation.

Ikiwa MP hatengenezi kazi yake vizuri, uchaguzi by - elections unafanyika.

Kitu kingine mambo ya nominated MPs yaondolewe kabisa!

Presidential candidates should be holders of at least Masters degree from a recognised university, a person of integrity with no criminal record of any kind. (clapping).

Tena, the powers of the Prime Ministers, the President should not be above the law. Rais wetu lazima awe chini ya sheria.

The Constitution should provide for the removal of the President when his government promotes corruption or when the economy of the country performs poorly for 2 consecutive years. (clapping).

Due to human factors, ikiwa uchumi wa Kenya umezolota kabisa kwa miaka miwili hivi, huyu President aondolewe, ama namna gani?

Kenyans should own land anywhere in the country. Ikiwa umebahatika kupata shamba mahali popote kwa nchi hii hakuna restriction ya kuishi huko.

Kitu kingine, after the budget, the district allocation for all districts should be published in the Daily Newspapers so that the public many know what services are expected from the ministries. This will minimise a situation where AIE holders and auditors collude to deny the public the services they need. Committee should be set at district level to monitor and verify from the public what the ministry has done according to the financial report.

Baada ya Budget. Last point – the President should be a Member of parliament. Mayors and Chairmen should be at least o-level holders with at least professional certificate from a recognised college. The MPs their qualification should be diploma

holders and above. The Constitution should provide free education in primary, cost sharing in secondary and free education in colleges and university.

Com. Maranga: Thank you very much.

David Bett: Utawala wa mkoa uondolewe kabisa.

Com. Dr. Maranga : David Bett, iwe ya mwisho. Sasa nipatie memorandum na uweke sahihi. Mary Cherotich, Mary, chukua mic utwambie darasa yako na shule gani unasoma.

Mary Cherotich: *Kainutikyuk ko Mary Cherotich.*

Translator: - Naitwa Mary Cherotich

Mary Cherotich: *Amiten class eight en sukulit ab Mugondik.*

Nasomea Mugodik Primary darasa la nane.

Mary Cherotich: *Ne tai ko kamache amwa ale kimache kewal somanet.*

Ya kwanza anataka system of education to be changed

Mary Cherotich: iwe 7-4-2-3 system na masomo ya primary iwe free

Com. Dr. Maranga : Eh endelea na Kiswahili.

Mary Cherotich: and secondary iwe cost sharing na university and colleges. Discipline in school should be equal according to the age.

Com. Maranga: Thank you very much. Come and sign. Injine ni Florence Chepkemoi, Florence kuja ongea kwa mic. Weka hio mic kidogo.

Chepkemoi Florence: *Kainutikyuk ko Chepkemoi Florence.*

Translator: - Anaitwa Chepkemoi Florence .

Chepkemoi Florence: *Amiten standard eight en Murwa dikrr primary*

Translator: Niko darasa la 8 Mugwondik primay school.

Chepkemoi Florence: *Ko kit ne amache amwa amache koik en Primary ko free education en sekondari ko cost shairing aak colleges and universities to be free.*

Translator: Napendekeza free education in primary , colleges and university and cost sharing in secondary.

Chepkemoi Florence: *Ak amache kisomeshan lagok tugul kokergeit tibik ak boys. Miten sigik che lazimishani lagokwak tibik koba tumdo ko matar somanosiekwak ko kounatet kemache kesomeshan lagok ko kerget.*

Translator:Amependekeza ya kwamba wasichana na wavulana wasome sawa na kabisa wasilazimishwe na wazazi kutahiriwa.

Chepkemoi Florence: *Ko kit na mache kora ko akoba mwalimuek.Mara komiten sukulit ne miten lagok bogol mutu ak mwalimuek mut kityo.kemache sikekerwech ingunon akoba mwalimuek ngot ko chang' lagok kemache mwalimuek che chang'.*

Translator:Amependekeza ya kwamba walimu wawe sawa Kenya ili kwamba wanafunzi ni wengi kwa shule fulani, walimu pia wawe wengi.

Com. Dr. Maranga : Thank you. Aweke sahihi – Dorcas Tembur

Dorcas Tembur: *Kainutikyuk kekurennon Dorcas Tembur.*

Translator: Kwa majina naitwa Dorcas Tembur.

Dorcas Tembur: *Ko kit ne kamache amwa ko ketaretwech sigik en maiwek chekiyeate en olono asi rabinik che katayeen maiwek ketaretech kisomesanech.*

Translator: Napendekeza ya kwamba serikali iangalie sana wazazi kwa sababu wanakunyua kunyua pombe na wanaharibu pesa ambazo wangetumia kusoma . Hiyo tu, ameshukuru sana.

Com. Dr. Maranga: Haya, huyu mwingine anaitwa Faith.

Faith Chepkurui: *Kainaiyuk ko Faith Chepkirui.*

Translator: Kwa majina anaitwa Faith Chepkurui.

Faith Chepkurui: *Ko kit ne amache amwa kemache koik Free education kongeten nasaret agoi eight en primary.*

Translator: Napendekeza free education in primary school,

Faith Chepkurui: *Ko en secondary kepyei*

Translator: kwa secondary school cost sharing,

Faith Chepkurui: *Ak en university ak college koik Free.*

Translator: colleges and universities to be free.

Faith Chepkurui: *OKo kimache kora serikali kotaret sigik en tuguk ab temisiet sikotaretech en sukul.*

Translator: I am also proposing that the government to give wananchi some tools to use in farming. Nimeshukuru.

Com. Dr. Maranga: Which class –

Translator: ako class 7.

Com. Dr. Maranga: Thank you very much. Tupate mwingine Richard Lang’at, Richard Lang’at, karibu halafu atafuatiwa na Kirui, Paul, kuna Kirui Paul, Kirui Paul, Kirui, Basi uwe tayari.

Richard Kipyegon Lang’at: *Kainenyun ko Richard kipyegon langat.*

Translator: Anaitwa Richard kipyegon Langat.

Richard Kipyegon Lang’at: *Ko chechuk komachang’*

Translator: Yangu itakuwa mafupi sana.

Richard Kipyegon Lang’at: *Oeng’ anan ko somok.*

Translator: Moja, mbili, tatu.

Richard Kipyegon Lang’at: *Kit ne kakimache kora en ng’atutik chuton kitau ko kamache amwea maoni ne nyun ne akenge.*

Translator: Ya kwanza kabisa napendekeza maoni yake moja kabisa,

Richard Kipyegon Lang’at: *Ne noton ko kobais sheria akenge ne katungani wanainchi cheba Kenya en Kenya mzima.*

Translator: kwa hivyo napendekeza sheria ifanye kazi ambayo ilitungwa na wananchi wote wa Kenya.

Richard Kipyegon Lang’at: *Makobais by-laws che kikonyanyasan bik che kebendi ingemure yeba wuyan kele by-laws ko kigosich ngamutik asikonyanyasanen wanainchi.*

Translator: Anakataa sheria ambayo inaitwa by-laws and Kangaroo Courts ambayo inatumika kunyanyasa wananchi.

Richard Kipyegon Lang’at: *Kimache sheria che ba emet ab Kenya ko akenge ma by-laws. Hiyo by-laws ikwishe!*

Translator: Sheria ya Kenya iwe ni moja na hiyo nyingine ya kangaroo courts iondolewe kabisa.

Richard Kipyegon Lang'at: I can show you one example

Translator: Example moja.

Richard Kipyegon Lang'at: *Ne tesetai en Transmara.*

Translator: ambayo inaendelea hapa Transmara

Richard Kipyegon Lang'at: ile kitu inaitwa nyayo,

Translator: ile kitu ambayo watu wanafuata mguu ya ng'ombe ambayo imeibiwa,

Richard Kipyegon Lang'at: asikuje kuniuliza mimi Richard Lang'at anataka kila sheria alinde, mtu asiache mali yake ipotee, akuje kwa Lang'at akaniuliza mimi ng'ombe yake.

Translator: I hope it is clear. (claping) amesema ya kwamba sio vizuri mtu alipe ng'ombe ambayo mwingine amepoteza, na sio yeye ameiba.

Richard Kipyegon Lang'at: *Ko kesame serikali, asikokimit ng'atutiet noton amun kitarenech tuguk.*

Translator: Anaomba serikali ihimize hio sheria, kwa sababu hio sheria ndio imemaliza mali ya Kipsigis hapa.

Richard Kipyegon Lang'at: *Ak konget serikali kosir asikarik si koteben barabara si makiime raia kelenji kobun yun tuga oko tinye serikali asikarik.*

Translator: Na serikali iweke askari kwa barabara ili iweze kulinda vitu vyenye vimeibiwa kama ng'ombe au mbuzi, ili watu wasikuwe wakiulizwa na wanalala usiku.

Com. Dr. Maranga: Asante Bwana Langat.

Richard Kipyegon Langat: Niko na moja, moja tu, Ya mwisho, *Atinye offisit ab Rais*

Translator: ya mwisho nagusia ofisi ya Rais.

Richard Kipyegon Lang'at: *Asikobit ketaret rais akine amaik greedy en boisiosiek.*

Translator: Rais asikuwe greedy, asipendeleo kila kazi, kila kazi,

Richard Kipyegon Lang'at: *Amun kibare kegerRais kouwon kagile kele rais kouwon kagile Kenya koma kimache kounon.*

Translator: kwa sababu tunaona vile huwa ni kwamba tukiona Rais, ni kama Tumeona Kenya nzima.

Richard Kipyegon Lang'at: *Kimache ke pie boisiosiek ak maministers , MPs of parliament ak DCs ak ko pitishan mamlaka ne tinye rais asikomako...*

Translator: The power of the President should be shared. Okey. Asante.

Com. Dr. Maranga: Lakini Bwana Lang'at nataka kukuuliza, kama nyayo inapotea kwako kila wakati lazima serikali itauliza wewe. Kama nyayo ya ngombe inafuatwa, inakuja, inaishia kwa Lang'at, inakuja, inaishia kwa Lang'at lazima utaulizwa.

Richard Kipyegon Langat: No, sasa nitajua aje na mini nalala? Aa, kitu nauliza, Bwana Lang'at, no, sio kuuliza, ni kuingia tu hata ngombe ikikuja mpaka mlango mimi nalala na watoto wangu kuamuka naulizwa.

Com. Dr. Maranga : Watoe hio ngombe kama exhibit, aende ashike vitu yake. (laughing) Aah – ooh ye, I had called you. You are Kirui Paul, I am Kirui Paul Johana Nge'no Kipyegon John ole Saitoti ambaye wameungana pamoja katika team moja inaitwa **KIMA** Alliance. Yaani, Kipsigis, Masai alliance na wameandika memorandum yao.

Kirui paul: The highlights ama areas ambazo tuliangalia sana katika hii matakwa tunaangalia leo. Ya kwanza kabisa ni kuhusu commissions ambayo inawekwa hii Tume, iangalie kwamba hiyo Tume imewasilisha matokeo ya hio Tume. Ili pesa mingi serikali iwekwe kwa Tume halafu baadaye isitoe hiyo results. Kwa sababu kuna Tume mingi zimewekwa na serikali kama Ouko enquiry Commission, kama ile ya Akiwumi Commission na hizo Tume pesa nyingi serikali iitumia na hatujapata results. Kwa hivyo hata hii yenu, hatujakuwa na imani sana kwamba mtatoa results. (clapping).

Ya pili, ningependa kugusia juu ya independence of Constitution Review Commission na election. Tumeomba sasa, tungewaomba ninyi, serikali ikuongeze muda au miaka miwili ili mukae polepole mchunguze ni sheria gani inafaa kubadilishwa, msikuwe na haraka lakini election tufanye tofauti. Election tufanye kwa wakati unaofaa lakini Constitution Review iendeleo hata kama itamaliza miaka kumi iendeleo kwa sababu hatutaki Constitution ambayo si ya kuharakisha. Unajua ukipika ugali na uharakishe, utoe kabla haija iva , labda unaweza kuwa mgonjwa. So we request independence ya Constitution Review na elections.

Ya tatu, pia ningegusia juu ya election of MPs tungependelea sana kwa wale wabunge wanachaguliwa wakiwa wamechaguliwa, kuwe na Katiba ya kusema kama mbunge amejihusisha na maneno kama ya raping, kama mbunge, anajihusisha na maneno kama ya uvumi, kama mbunge amejihusisha na maneno ya corruption, wakataliwe wawanie “kiti” cha

mbunge. Ili tusikuwe na wabunge ambayo wanaenda kuwanajisi. Watoto, kuwanajisi yaani, wanafanya madhara sana na kutungwe Katiba ya kwamba wakati mbunge amefanya vitendo kama hivyo. There should be a Constitution ambayo inanyanyasa huyo mtu a resign immediately akipatikan kwamba amefanya vitendo kama hivyo.

Pia ningependa kuomba Administration police should be merged with police. Hiyo neno ya administration police iondolewe kabisa. Administration Police wakae kama polisi ili tukuwe na police of Kenya tu peke yake. Hii ma Administration Policemen wako corrupt sana na wanatumiwa na D.Os na ma D.Cs and assistant chiefs kufanya uhalifu Kenya hii. Kwa hivyo waondolewe tukuwe na polisi wa Kenya ambao wamesomea sheria.

Com. Dr. Maranga : Ya mwisho!

Kirui paul: Pia ningependa kuomba, ningependa kuomba chiefs, kama ni lazima kuwe na chiefs, should be transferred. Wawe watu wanapigwa transfer kama waalimu, polisi, ili wakikosea pahali, wanaenda, North Eastern, wanaoneshwa discipline huko.

Com. Dr. Maranga: Asante Bwana Kirui, N.Eastern ni sehemu moja ya Kenya hata watu wa North Eastern wako na raha yao, kwa hivyo hapo hakuna discipline – (Laughing.)

Com. Dr. Maranga : Your last point.

Kirui paul: My, my last point ni kuhusu lands. Unajua Kenya hii kuna kitu ambayo inaitwa adjudication sections . Tungependa serikali iondoe hiyo sheria ya kusema ati a section has been declared, inaitwa section wakamati fulani, makamati wanachaguliwa, hiyo kamati inakuja kusumbua wananchi. Tukuwe na Katiba ya kusema kwamba kama shamba hii inakatwa inakatwa ikiwa Chairman mwenye shamba na adjudication officer. Tusikuwe na hizo kamati nyingi na kufanya maneno mengi.

Kuhusu mipaka, kuna mahali inasema, there are some communities ambayo wanahitaji ile mpaka ambayo iliwekwa na wakoloni e e tulionelea, sisi kama wa Kipsigis hata na sisi pia tulionelea hiyo mipaka ikiwa reviewed, wakoloni ambayo inatokea sijui Laikipia inaenda Narok inaenda mpaka Tanzania. Hiyo mipaka ikiwa reviewed, tukirudia tutawaodoa watu wengi sana, tutawaondoa wa Masai wote waende, na hatutaki tufanye hivyo. Tunataka sheria ambayo inasema yule mtu anakaa kwa ile mahali anakaa, akae kama amepata shamba kwa njia ya harari. So we should not refer to those mipakas.

Com. Dr. Maranga: Thank you very much asante Bwana Kirui.

Kirui paul: Kwa majimbo ningesema tunakataa maneno ya majimbo.

Com. Dr. Maranga: Weka hio memorandum. Weka sahihi hapo. Tupatie memorandum. Ee Josea Chirchir – Okey.

Joseah Chirchir: Upande wa jina ni Joseah Chirchir. Mambo yangu ya kwanza ni kuhusu kortini. Kortini lazima ajitawale ikiwa hakujakuwa na Judge mkuu katika Kenya korti awe na msimano yake peke yao. Asiwe anakataa kwa mtu fulani ya kuamrisha.

Vile vile kabla mimi sijaondoka, wakati wa kuhitimu, kuna kitu ya wakati wa kuapa anatumia Biblia, na labda saa ingine huyu mtu amefanya dhambi, ameuwa mtu na anachukua Biblia juu kusema nitasema kweli, iko kweli wapi? Kila kabila itumie ile kitu ilikuwa inatumia zamani. Kama Kipsigis alikuwa anatumia nini kwa korti, kama Wakisii atumie vitu yao. (Kipsigis dialect). Na Wakisii nasikia walikuwa wanatumia miti inaitwa (Kisii name). Atumie hiyo. Biblia iwachie kanisa kwa sababu ni neno la Mungu.

Neno lingine ni kuhusu watoto wetu. Kama msichana kwa mambo ya shamba ikiwa hajaolewa, apate shamba sawa na kijana. Na unajua wakati mwingine kijana ya jirani akiona amepata shamba anataka kuo a yeye na akiolewa awache shamba ya baba, aende kupata shamba huko.

Jambo lingine kuhusu wasichana. Kijana anachukua wasichana, watoto ya watoto wetu, anakwenda kaa naye mwezi tatu anapunguza, kwenda na nilikuwa namwambia nitaoa natakiwa Katiba inasema yeye akichukua wiki tatu, awe mke wake. Na kama anataka kaa na yeye kidogo, akae wiki mbili tu. Lakini ikiwa wiki tatu, awe mke wake. Kwa sababu amesumbua (Kipsigis dialect).

Neno lingine ikiwa kwa hapo tena ikiwa kuna talaka na mwanamke wangu anataka ondoka na awe na watoto tano, lazima hii watoto igawe, mwanamume ibaki na watoto tatu nae aende na watoto wawili kwa sababu atakwenda zaliwa wengine na mme mwingine.

Com. Dr. Maranga: Haya asante mzee. Hio ndio point ya mwisho. Haya ya mwisho!

Joseah Chirchir: Hii ndio ya mwisho kwa sababu wewe umekatalia. Ilikuwa sita. Ni kuhusu utajiri ya nchi kama district. Lazima tugawe utajiri ya wilaya. Kama kuna Chai kama Kericho, kama hii wanyama wa pori wanatumwiwa na Wamasai, pesa peke yao, hii ni mali ya wilaya. Lazima kila mtu ambaye yuko hapa apate na kuajiri watoto tena ni utajiri ya district. Kila watoto waajiriwe kulingana na uwezo wake ya masomo. Sio kuchukua mtoto wa Masai ambayo ni ya darasa la saba na wengine anasema Kipsigis. Sisi tutakwenda wapi, na tunaishi hapa?

Neno langu la mwisho ni kuhusu utajiri wa nchi nzima. Inatakiwa kwa uchumi Katiba iseme natakiwa kila mtu awe afadhali. Ikiwa minister anatumia gari kama ile, lazima mwananchi atumie Toyota ili aonyeshe ile utajiri ile ya gari, mwananchi yake ile

anaongoza wako level ya anatembea na gari kuliko mimi natembea na miguu na mtu anatembea na Pajero na inakuwa maskini.

(clapping)

Com. Dr. Maranga : Okey, asante mzee wangu. Asante nashukuru, hio maoni tumesikia sana.

Josea Chirchir: Ijapokuwa wewe umemaliza mimi.

(laughing and clapping)

Com. Dr. Maranga: Kuja weka sahihi hapa. Huyo mzee wangu anasema nimenkatisha na kuna wengine wengi wako na mazuri kama yake. Au namna gani? Si kila mtu apate nafasi? Richard Maritim, Richard Maritim, hayuko? Ako wapi? Halafu atafuatiwa na David Bett, David Bett ako, basi uwe tayari. Fupi fupi na mzuri.

Richard Maritim: Majina ni Richard Maritim. Ningetaka kuanzia uzito ya Rais. Rais asiwe na uzito kama wakati huu.

La pili katika uchaguzi wa councillors Chairman, wananchi wawe wakichagua Chairman.

La tatu, watoto wasome free kwanzia darasa la kwanza mpaka secondary.

La nne kila mtu ambaye anaishi apewe cheti cha kumiliki shamba.

La tano katika wilaya yetu, resources ambaye inapatikana igawe kwa wilaya hio hio kulingana na watu ambao wanaishi hapo hapo.

Ya sita, katika uchaguzi, kila polling station ihesabiwe kura, sio kupelekwa kwa wilaya. Kwa kila polling station, ihesabiwe. Ni hayo tu.

Asante mzee wangu, weka sign David Bett atafuatiwa na Samuel Kigen, Samuel Kigen ako, basi uwe tayari. David Bett, na wewe ni David Bett, Box yako namba ngapi, yes, wewe ndio huo. Yah.

David Bett: Asante sana. Langu la kwanza ningependa kusema aah Kwa majina mimi ni David Bett – kwanza kabisa ningependa kusema ya kwamba kila district iwe na at least 3 constituencies na watu ambao wanawania kitu ya ubunge kwa hiyo constituency, provided tu awe na qualifications ile inatakikana, mtu yeyote hapa anaweza kuania kiti ya ubunge.

Pili, ni land issue. Nasema ya kwamba kila Mkenya ana uhuru kuishi mahali popote Kenya ambapo atakuwa amepata Shamba.

Na serikali ilinde yeye mahali ako.

Tatu fundamental rights – security ya watu, wananchi iwe juu ya serikali. Na bunduki zote zinazomilikiwa na raia zichukuliwe na serikali peke yake iwe na bunduki.

Na majimbo, ninakataa. Election date, tarehe ya uchaguzi iwe inajulikana na kila mwananchi. Kama ni leo inajulikana even after 10 years. Kama hata baada ya miaka 10 tuwe tunajua mwaka wa 2015 tutachagua, tutafanya uchaguzi tarehe fulani.

Na salaries, tuwe na Tume huru ambayo inachunguza salary ya wafanyi kazi wa serikali wote. Sio Mps waangalie maneno yao ya salary. So we are saying tuwe na independent Commission ambayo inachunguza salaries.

Na compensation, hapa tuko na wild animals in our district na kila siku hawa wanyama wanauwa watu wetu na compensation hatuoni. Na kama iko ni kidogo sana. Ninasema kuwa compensation ya mtu ambaye ameuwawa na mnyama iwe one million hata zaidi. (clapping)

Na ya mwisho ni elimu, nataka kusema kwamba elimu iwe free kutoka nursery mpaka form four, sorry mpaka secondary, iwe cost sharing, universities and colleges iwe free na walimu wa nursery iwe juu ya serikali na wazazi wasisumbuliwe na kulipia hawa.

Com. Dr. Maranga: Asante, thank you very much Bwana David Bett. Samuel Kigen,

Samuel Bett: Asante sana. Kongoi missing.

Com. Dr. Maranga: Hebu ngoja kidogo, tangazia watu. Hujui Kiswahili mzee, anza kwa jina.

Translator: *Kamache aparastechi bichon kaitu alenji osigei en yono okot ngot ko me ng'alale ke machesikenai kele bik ata che ka mi yu. Isire kei en yon ak imwa ile mang'alale anan ang'alale. Kongoi.*

Samuel Bett: Kwa majina yangu mimi naitwa Samuel Bett arap Kipyego. Kitu mimi nataka kupendekeza, moja tu ama mbili ni kuanzia nyumbani, mimi ni kuanzia nyumbani tu kwa sababu mambo yangu yako tu hapa nyumbani. Nilikuwa nataka kusema mambo ya Chief, sub-Chief wachaguliwe kutoka hapa nyumbani kwa sababu hio ndio mtu mnaifanya kazi pamoja, mnaishi pamoja, tena ni jirani. Na kama anakuja kuandikwa na wengine wanatoka mbali, hawezi kujua kama huyo mtu anafanya kazi hapa namna gani sasa tunataka iwe tunachagua kutoka nyumbani. Na hiyo kazi yote inaenda vizuri.

Tena naomba mambo ya sheria irekebishwe namna hii tena. Tushukue kazi moja, mtu moja kazi moja mtu mmoja hapa Kenya.

Hapana wewe unakuwa Chairman ya sukari, Chairman ya barabara, Chairman ya miwa, Chairman ya chai, sasa na wewe tu moja, na pesa inatoka tu kwa hiyo mtungi moja na wewe peke yako unapeleka kwako! Na yule mtu hapati ata kitu, yuko mtu anakaa bure tu, ndio mimi nasema mtu moja aangaliwe afanye kazi angalau na wengine wapate. Hiyo ndiyo pendekezo yangu.

Com. Dr. Maranga: Asante mzee, asante. Na uweke sahihi, ile meza yetu ya chini huko nyuma. Gideon Terer, Gideon, Sasa mimi nataka watu watoe maoni kwa haraka kabisa. Watu ni wengi. Gideon Terer, dakika moja moja, watu watoe ile maoni ya muhimu.

Gideon Terer: Kwa majina naitwa Gideon Terer nataka nitoe maoni yangu kuhusu Katiba ijayo. Nataka kuanzia ofisi ya Rais. (inaudible).

Gideon Terer: Point yangu ya mwisho ni hii maneno ya NHIF. Vile nimeona, hata ingawa NHIF laws imebadilisha kidogo, haitahusu yule mwananchi yuko mashambani kwa sababu iko hospitali ambayo inasemeka na, ni recognized. Hatuna hapa, tunaingia tu kwa ile private hospital na tunataka hata ifike chini hizo NHIF forms. zitumike kwa hospitali kidogo.

Com. Dr. Maranga: Asante mzee wangu –David Gideon Terer, tunataka David Kipngetich, Okey, sasa kwa nini ulikuwa unajiita David Bett, hata hujaandika hivyo, umeandikwa David Kimngetich.

Com. Dr. Maranga: Okey endelea basi.

David Kipngetich: Mine, I will talk in English. I have some proposals. Parliamentarian should be someone who is an educated person. If his development plan is doomed, he/she should be voted out.

He/She should draw action plan. Coucillors also should be educated.

Com. Dr. Maranga: Endelea, Ongea

David Kipngetich: Ya sita, wealth must be divided as per the population. Locations should be divided as per the population.

Chief or Assistant Chiefs must be literate. He/She should be able to communicate both in English and Kiswahili properly.

The government should be unitary.

Education must be compulsory to all school going children.

Everybody must educate his/her own children.

People must be given opportunity to educate their own children.

Now, corrupt officers must be fired from employment.

Hotline should be a communal utility.

Com. Dr. Maranga: Thank you, last point!

David Kipnetich: Income from the natural resources in the district should be distributed equally among all the peoples living in the district.

Decentralisation of power – local government becomes autonomous to make decision on its own and implements even if it is to have more than one Constitution.

Constitutional chiefs and government departments on infrastructure on the district, that one should be the responsibility of the government.

Com. Dr. Maranga: Asante sana mzee David, sasa nipatie memorandum na uweke sahihi ile register yetu. Chini. Rotich Paul, Rotich Paul, hayuko. Rotich Paul, wewe unatoka pande gani? Anyway kuja ongea. Wewe ni Rotich! Na atafuatia na Daniel Soi – bado, uwe tayari. Dakika moja peana maoni ile ya muhimu.

Rotich Paul: My proposal – nataka Chiefs wawe watu ambao wamesoma, kufikia kiwango cha form 4 na wawe wamepata C and above.

Secondly, councillors wawe vile vile watu ambao wamesomana wamehitimu, wamefikia kiwango cha form4 na wawe na C and above also.

Na nominated councillors should be eradicated.

Thirdly, the Chairman of the County Council should be elected generally and should be holding a degree from a recognised university.

Independent Electoral Commission – some should have a Judge na Commissioners wateule na bunge in relation to the party prevailing in Parliament.

Number 5, the land issue, everybody should leave anywhere in the country, irrespective of the tribe.

Number 6 ni kuhusu mambo ya pesa, wanasisia ambao wanatumia pesa katika campaign wanafaa kupigwa marufuku, or there should be a law providing that anybody contesting for any constituency should not be using money to buy the votes because that will encourage corruption in the country.

Com. Dr. Maranga: Okey, Thank you very much: I also have one concerning the Attorney General. The Attorney General should be a legal advisor to the parliament and not to the government and the office of the Attorney General should be under Judiciary and the Chairman of the adjudicator should be elected by parliament or a parliament should take a Commission that will receive applications from persons willing to go for that post.

Com. Dr. Maranga: Thank you very much. Hand over your memorandum. Please come and sign our official register. Daniel Soi, Unajua sababu naita watu mapema ili wawe karibu. Sasa mimi nataka anaitwa Mashaidi Kirui. Aanza kwa majina yako.

Daniel arap Soi: Majina yangu naitwa Daniel arap Soi

Com. Dr. Maranga: Endelea mzee wangu.

Daniel arap Soi: *Kit ne kamache en Katiba ni impya neba nguni,*

Translator: Kitu ambacho nataka kwa Katiba mpya hii inaendelea sasa hii

Daniel arap Soi: *Ko en kanisosiek tugul ko nyalu kerigistan kobunji iman age tugul, ma mi ne kowon*

Translator: Mekanisa yote Kenya yawe registered na yote yasemekane ni ya ukweli.

Daniel arap Soi: *Ng'aliot age ne kamache en Katiba neba nguni,*

Translator: Kitu kingine nataka kwa hii Katiba ya sasa,

Daniel arap Soi: *Kong'eten en wabeberu mpakaKenyatta agoi inguni ko mi bik che tom konam Tittle deed ago kerke ak igo ko kilyan.*

Translator: Tangu wakati wa Ubeberu, tangu wakati wa Kenyatta, tangu wakati wa sasa kuna watu ambao hawajapata tittle deed. Kwa nini?

Daniel arap Soi: *Ako inguni iwalegei bichutan ba emani ko kimengik ab emani.*

Translator: Na sisi watu wa area hii jinsi vile tulivyo Kipsigis, sisi ni watu wa area hii,

Daniel arap Soi: *Ko kit namache en Katiba neba nguni,*

Translator: sisi tunataka katika Katiba ya sasa,

Daniel arap Soi: *En bik ab Transmara*

Translator: sisi watu wa Transmara,

Daniel arap Soi: *Konyalu kotak tugul kobik che akenge.*

Translator: Watu wote wawe sawa.

Daniel arap Soi: *Mami bik alak che kimuche ke chil en kebeber.*

Translator: Wengine wasifinywe kwa pande huu ama ule.

Daniel arap Soi: *Ak kisto kora in ng'atutiet age ne kirakas kele bik che kitebi squatter en emet en Rift Valley.*

Translator: Na hii sheria ya squatters iondolewe kabisa, nasikia kuna squatters Sehemu zingine.

Daniel arap Soi: *Rift Valley ko emenyon.*

Translator: Rift valley ni yetu

Daniel arap Soi: *Komanyalu ko mi chito ne ba Mombasa ne nyokosiche Tittle deed ko neba Rift Valley komatinye.*

Keguren Squatter.

Translator: Na unawezapata ya kwamba mtu ametoka Mombasa na ako na tittle deed na mwenyenji mwenye amekuwa hapa hajapata hiyo title.

Daniel arap Soi: *Ko kit ne kamache ingunon agane en Katiba neba inguni, amun angen ale imuche kotar kenysisiek mia mbili si kesich.*

Translator: Kitu anataka kuwaita sasa kwa hii Katiba sasa itachukua muda sana kama miaka mia mbili.

Daniel arap Soi: *Ko kamache sio ker otaretech.*

Translator: Muangalie sana halafu mutusaidie.

Com. Dr. Maranga: Nashaiki S Kimojiro.

Coucillor Ole Kimojiro: Mimi kwa majina naitwa coucillor Ole Kimojiro,

Com. Dr. Maranga: sio Mashaiki,

Nashaiki S Kimojiro: Nashaiki ‘ S ’ katikati. Ningetaka kutoa maoni yangu kuhusu wanyama wa pori na binadamu. Wanyama wa pori wamemaliza watu kuuwa, lakini inaonekana kuna sheria haijalinda binadamu. Kwa sababu mnyama akiuwa mtu inalipa binadamu elfu thelathini. Na inachukua muda wa miaka kumi au kumi na tano ilipwe hio fidia. Hiyo irekebishwe na iangalie binadamu sawa sawa kwa sababu ukiona familia ambayo imeuliwa na wanyama wa pori, ni wengi na mpaka saa hii haijaripia fidia.

Ningependa kutoa maoni kuhusu lodges. Lodge katika Masai Mara Game Reserve. Masai Mara Game Reserve tuko na ma lodges mengi na ningependa Katiba ambayo inatengenezwa ichunge wale watu ambao wanapakana na hizo lodges kwa sababu ukienda lodge utapata locals hajaajiriwa na huko ni mahali ambapo angeajiriwa. Kwa sababu ukienda lodges utakuta 95% ni wageni kutoka mbali lakini sasa 10 ni local. Kwa hivyo hio Katiba ingerekebishwa. Local people ambayo inapatana na hizo ma lodges iandikwe 75% halafu 25% iwe wageni.

Ya mwisho kabisa ni mambo ya mashamba. Adjudication section ikifunguliwa na kukatwa kwa yule mtu anapata shamba huko hio wazee wa adjudication board ndio wanaamua kwa sababu watu wa lands wamekuwa watu wa biashara hata Transmara imetangazwa Lands ndio iko corruption kushinda karibu dunia yote nchini. Kwa hivyo wazee, adjudication board ipatiwe nguvu na waamue kesi kama kuna ubishi. Thank you very much.

Com. Dr. Maranga : Asante councillor: Sasa watu tafadharini, mushike wakati mje hapa mkitoa yale maoni pengine umesikia hayajasesemwa sana. Milta ? Milta chemutai? Sijui ni jerita ama ni cheritai? Hebu pengine atatwambia jina yake kamili. Una dakika moja mzee wangu.

Michael Nepore: Naitwa Michael Nepore ole Pirde.

Com. Dr. Maranga: Sio yeye basi,

Michael Nepore: Ni mimi yule aliandika ndiye hajui

Com. Dr. Maranga: Basi ni wewe.

Michael Nepore: Mimi natoa tu oni moja. Katika hii Transmara, tuko na community karibu nne. Lakini kwa division ya Kiridon, tuko na community ambayo ni kubwa kushinda wengine. Na hio community inataka kumeza wale wengine. Ningependa wakati inaundwa sheria, serikali ilinde community ndogo ndogo na hata watengenezee sehemu za uwakilishi katika county council. Ingawa basi kama hawezi kupata kwa masehemu katika MPs basi katika county council yaani ma community zote ambaye ni kidogo katika jamhuri ya Kenya wapate ata angalao waakilishi katika County Council ili utawala wote katika

Kenya yafikie basi makabila yote wakubwa pamoja na yale madogo. Niko na hiyo moja tu.

Com. Dr. Maranga: Asante mzee wangu. Basi watu wafuate mfano wa mzee unaona anaweka point kamili. Joshua Rongai, Joshua Rongai, haya Karibu.

Joshua Rongoe: Kwa majina mimi naitwa Joshua Rongoe na ningependa nitoe maoni kuhusu serikali ya mitaa na serikali kuu. Mini ningetaka serikali kuu iendelee katika serikali ya mitaa. Halafu serikali ya mitaa ijisimamie yao peke yao. Halafu ile pesa inapatikana kwa serikali ya mitaa isaidie wananchi kujenga mashule.

Jambo la pili, ni mali asili yetu. Mimi nataka serikali ichunge mali asili yetu kwa sababu hapa Kenya sehemu kubwa inafurugwa na wanyama wa pori lakini hakuna hatua yeyote inachukuliwa na serikali. Na mimi nataka Katiba ichunge halafu ikiharibiwa na wanyama, idara ya kungalia wanyama, waangalie na walipe wananchi.

Lingine ya mwisho ni mahakama. Mimi nataka mahakama, kuwe na mahakama ya kufanya kesi ya corruption. Kwa sababu na hio ma kesi ya mahakama isimamiwe na mkuu wa sheria. Na mkuu wa sheria ichaguliwe na bunge, sio kuchaguliwa na Rais.

Jambo lingine la mwisho kabisa, kabla ya uhuru kulikuwa mapatano kati ya serikali ukoloni na Wamasai. Na hio mapatano ilikuwa inasema ya kwamba Wakoloni wakiondoka, Wamasai warundishiwe shamba yao. Na mimi nataka hio Katiba ifanye kazi Wamasai warudishiwe shamba zao. Mimi nafikiri ni hayo tu.

Com. Dr. Maranga: Thank you very much. Weka sahihi. John Korir. John Korir, John Korir! Halafu atafuatiwa na ..huyu ni nani ?

John Korir: Jina langu ni Bwana John Korir. Kwanza our Constitution, lazima iwe na Preamble na Preamble kwa maoni yangu, napenda iwe namna hivi: “ We the people of Kenya do hereby uphold the Constitution for a prosperous nation as enshrined in the court of arms and the national flag. May God bless our nation”.

Mambo ya mashamba: Kuhusu mambo ya mashamba ninapendekeza ya kwamba kila mwananchi awe na haki kupata au kununua shamba mahali popote katika jamhuri ya Kenya. Na ni jukumu ya serikali alinde yeye pamoja na hio shamba pamoja na mali yake.

Pili, kuhusu mambo ya shamba pia, napendekeza ya kwamba wavulana na wasichana wawe na haki ya kumiliki ardhi.

Tatu, napendekeza ya kwamba mapatano ambayo makabila wengine walipatana kuhusu mambo ya shamba hio iendelee kwa sababu hio inagawanya nchi na vile vile ilikuwa mambo ya ukoloni ambayo inatenganisha wananchi. (clapping).

Kuhusu mambo ya County Council – Local government napendekeza ya kwamba mwenyekiti au mayor achaguliwe na wananchi directly na awe na elimu ya juu hasa kutoka kidato cha nne na juu.

Na vile vile napendekeza ya kwamba serikali au Local Government awe na authority – nasema ya kwamba yule mwenyekiti awe na power yaani, Central Government hawezi kuwa na power yaani Treasurer, na clerk anyang'anywe power na councillor apatiwe power.

Com. Dr. Maranga Last Point:

John Korir: Vile vile kuhusu mambo ya elimu napendekeza ya kwamba walimu wa Nursery waajiriwe na serikali na vile vile elimu iwe ya bure kutoka nursery hadi darasa la saba na vile vile kwa secondari iwe cost sharing. Na higher education mpaka university iwe free.

Na pia napendekeza ya kwamba watoto walemavu wapatiwe free education kabisa. Kutoka nursery hadi university – free

Vile vile, education iwe independent na to be held by professionals. Na Teachers Service Commission iwe established kwa mambo ya Commission and vile vile walimu walipwe mishahara, wawe competent to apply competent services. Thank you .

Com. Dr. Maranga: Asante sana. Naona wewe uko na memorandum tutasoma na uende uandike halafu utupatie. Samuel Koskey, Samuel Koskey, karibu.

Samuel Koskey: Kwa majina naitwa Samuel Koskey kutoka hapa Transmara. Maoni yangu la kwanza kabisa ni kuhusu ardhi. Mtu atakapomiliki ardhi zaidi ya miaka 12 ana haja ya kupewa hati ya kumiliki.

Kuhusu elimu: Elimu iwe ni bure kwa wote. Kutoka darasa la kwanza hadi la nane.

Kuhusu mishahara: Mishahara ijandiliwe kwa pamoja kwa sababu wabunge wanapojipangia mishahara yao na mara ni tofauti na watumishi wa umma wengine?

Polisi, polisi lazima wawe ni kikosi kimoja. Wasitenganishwe kusema hawa ni polisi wa kawaida, polisi ya utawala, kwani kuna utawala gani tofauti na serikali iliyoko. Kuna wananchi wataaliwa na wengine hawataaliwi, kwa hivyo lazima polisi wawe ni kikosi moja tu waitwe ni polisi, sio kusema ni tawala wa ziada na nini, wa ziada wanafanya kazi gani hio waziada wanafanya kazi gani ni uhalifu huo! Kwa sababu ziada ni uharifu? Sio utumishi kwa uma tena.

Kuhusu ndoa, mwanamke akitengana na mumewe zaidi ya miaka miwili, apewe talaka kulingana na sheria. Kwa wakati huu

kuna magojwa mengi mwanamke anapoenda zaidi ya mwaka moja ina maana atakuletea madhara mengine tofauti.

Na watoto wengine tofauti, sio sura zako, na anasema wote ni wa kwako na hari wamezaliwa na wakisii na Wanandi kule ndani. (laughing)

Wasomi: Elimu kazi zote ambazo zinapatikana kutoka kwa serikali lazima zilingane na elimu mtu anayo mpaka kidato cha nne.

Com. Dr. Maranga: Last point.

Last point nasema ma chief lazima wamechaguliwa na wananchi na kama hawachaguliwi na wananchi wapigwe transfers kama wafanyi kazi wengine wa serikali. Sio akae zaidi ya miaka 12 na nikikosana na mtu tena mimi atanidhuru maisha yangu yote na uongozi wake.

Com. Dr. Maranga : Thank you very much. Peana hiyo memorandum. Pita pande hiyo ndio ukakuje ukakate mawaya hapa. Kirono Soi, Kirono Soi , Kirono arap Soi, kuja hapo halafu John Juma, John Juma ako! You will be next.

Kiprono Soi: Kwa majina naitwa Kiprono Soi, mimi ni mkaazi wa hapa. Pendekezo langu la kwanza ni kuhusu ardhi. Mimi nalipendekeza ya kwamba mwananchi aliishi mahali popote katika nchi yetu ya Kenya bora tu awe mukaazi.

Pendekezo lingine kama mtu amekaa mahali fulani, kwa nini Title deed zinakawia kama mtu amekaa miaka 12 na zaidi title deed zitolewe haraka sana iwezekanavyo.

Jambo lingine ni kwamba hawa watu wenye kusema majimbo, mimi nasema majimbo yaondolewe katika Kenya ya sasa, kama ilikuwako, ilikuwa ni ya ukoloni.

Tunataka Kenya mpya na Katiba mpya. Katiba ilinde kila mtu pahali popote na jambo lingine ni kwamba kuna sheria katika Transmara hii ya wizi wa ngombe ilikuwa mtu moja amesema; ilipendekezwa ya kwamba ilikuwa District ya Bomet, Kericho, na Kisii na Transmara walikutana siku ingine ikasemekana ngombe ilindwe. Lakini ikabaki Transmara Peke yake inalinda, Bomet hawalindi. Na Kisii, ng'ombe ikienda Kisii hawalipi. Kwa nini imebaki Transmara peke yake? Nalipendekeza hio kitu ipotee kabisa isionekane kwa sababu ni kunyanyasa wananchi.

Com. Dr. Maranga : Thank you very much asante mzee wangu.

Kiprono Soi: Jambo lingine ni kwamba hii kusoma, masomo ya watoto, nalipendekeza mtoto asomeshwe mpaka secondary halafu sasa ikifikia huko university tutakuwa cost sharing na serikali.

Com. Dr. Maranga : Asante. Weka sahihi, eeh Juma, John Juma, apana, sema Kiswahili wewe unajua.

John Juma: Kwa jina naitwa John Juma mimi ninaishi hapa Trasmara. Nafikiri jambo la kwanza ningependa kuongea ni kuhusu majimbo. Kuhusu Majimbo tunaona ya kwamba majimbo yakitokea yanaweza kuleta ukabila na kutawanya watu kwa njia mbali mbali. Kwa hivyo ningependekeza ya kwamba Majimbo yapotee kabisa.

Tena jambo la pili, ni kuhusu uchaguzi, uchaguzi wa Rais ama Katiba ambayo inaendelea kwa wakati huu. Ninaonelea ya kwamba uchaguzi uweze kufanyika mwaka huu halafu kama Katiba itaendelea kurekebisha pole pole kama uchaguzi umefanyika.

Jambo la tatu ambalo nitamalizia ni ya kwamba kuhusu vile watu wanaweza kuishi katika Kenya. Katika Kenya ni vizuri mtu aishi pahali popote na kama anaishi mahali popote aruhusiwe kwa sababu ukizuiwa uwambiwe kwamba huwezi kuishi hapa, huwezi kununua shamba mahali fulani, au huwezi kugombea kiti cha ubunge mahali fulani, ama councillor, hapo inaonekana ya kwamba kutakuwa na ubaguzi. Kwa hivyo ninonelea kwamba kila mtu aishi mahali popote. Kama ni kununua shamba ununue shamba mahali popote kwa sababu ukizuia inaleta ukabila.

Com. Dr. Maranga Charles: Asante sana Bwana Juma, Thank you very much

John Juma: Kwa hivyo kila mtu aishi mahali popote, asante sana.

Com. Dr. Maranga: Asante. Basi weka hiyo memorandum, na uweke jina yako na u sign register yetu. Koskey Daniel, Koskey Daniel.

Koskey Daniel: I am Koskey Daniel. My proposals are, I am going to touch on the Executive.

Com. Dr. Maranga : You have one minute to give us the main points.

Koskey Daniel: Now, the power to declare state of emergency that is granted to the President must be approved by $\frac{3}{4}$ of the parliament within 4 days of the declaration to ensure that improper or dubious security zones are not declared anywhere in the country.

Secondly conscious of the fact that a President has many opportunities to make money outside unknown places, the proposal mandates that the President must declare his/her wealth and sources of that wealth as such of the nomination process.

Income received as President is part of the public records and EAC has no control over government land and property.

Another issue is this is about 'Busaa' Busaa should be legalised or else this one from industries should be scrapped off.

Another thing is about the currency. We have got this money. At times we have seen the head of President. It should be removed from the currency.

Com. Dr. Maranga: Thank you very much Bwana Koskey. You can give us your memorandum. Yule ambaye anafuata sasa ni Jackson Ngok. Jackson Ngok?

Jackson Ngok: Thank you very much. My memorandum, the first one is everybody is free to settle anywhere in Kenya.

Com. Dr. Maranga: Aanza kwa Majina.

Jackson Ngok: My name is Jackson Ngok. A Commission should be set up to oversee the creation of constituency. You can find some areas which have got less population has got so many constituencies but ours here we have got more than 100 000 people and we have got only one Constituency. This is unbalance regional development.

Com. Dr. Maranga: Ongea Kwa Mic.

Jackson Ngok: Provincial Administration should be taken on its own should be taken by the local authority which is very close to wananchi. Chairman and mayors of the Local Authorities should be elected directly by the Wananchi.

Local councils should be given more powers to manage the local resources.

The new Constitution should state and give direction to finance states and provide facilities.

Any elected leader who has messed up should be voted out under impeachment. You can find President anaweza enda district zingine anatoa millions ya pesa na anasahau district ingine.

My last point, village elders should be in the government payroll.

Voter registration exercise should be continuous.

Majimbo system should not come in. Thank you very much.

Thank you, you register now. Councillor Stanley Cheruiyot:

Stanley Cheruiyot: Kwa majina mimi naitwa Stanley Cheruiyot – Councillor kutoka Murgan. Kwa mapendekezo yangu, ningeanzia mambo ya Commission. Electoral Commission wawe wakimaliza kazi yao kutoka kwa polling station, sio kwa district.

Ya pili, ni kuhusu natural resources. Ningependa vitu kama msitu, na wanyama ya pori seikali itunze.

Inginge KWS mimi nataka iondolewe kwa sababu imesubua wananchi. Wanyama wanaweza uua mtu na anachukua miaka 10 hata 20 bila ya kulipa kwa hivyo asiwasubue watu wetu. Wacha atoke ili wananchi wawe free.

Complaint nyingine ni security: Mambo ya security tupewe – tukiwa Transmara wako watu wengine wanapewa vitu ya kujilinda na wengine hatuna. Kama ni hivyo, tupatiwe kila moja tukiwa wananchi wa Transmara ama ichukuliwe hizo vitu, vitu kama ni bunduki, na vyombo vingine.

Jambo lingine ni mambo ya kortini. Sasa hivi, mambo ya kuwekwa mtu cell kwa miezi mitatu au mwaka moja iondolewe. Mtu akishikwa na makosa, aende direct akapigane na judge yake, akifungwa afungwe. Akifaulu, akuje nyumbani.

Ya mwisho ni mambo ya shule – Secondary school mambo ya Board of Governors katika Secondary School itolewe. Wananchi wa hio shule wachague mambo ya Board of Governors. Sio Kwenda kuchaguana pahari pengine. Ni hayo tu nilikuwa nayo.

Com. Dr. Maranga: Asante Councillor, nimekupa muda mrefu kidogo, wewe ni kiongozi. Benjamin Kerer, Benjamin Kerer, wapi yeye? Kuja, haya yule anafuata ni David Otieri, David Otieri ako? Uwe tayari. Mzee una dakika moja utoe maoni yako muhimu.

